**UTANGULIZI**

Mnamo mwezi Machi 2009, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya marekebisho katika sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973 na kupitisha azimio la kuruhusu pikipiki za magurudumu mawili na magurudumu matatu kuwa moja ya vyombo vya usafiri vilivyoruhusiwa kutoa huduma ya kubeba abiria kwa malipo au kwa kukodishwa.

Sisi Bodaboda wa Wilaya ya Arusha mjini tunaofanya biashara ya usafirishaji wa abiria kwa pamoja, tumeamua kuanzisha umoja wetu ujulikanao kama (UBOJA) Mwezi January 2017. Umoja huu utaongozwa kwa mujibu wa Katiba hii kama nguzo na d

ira yetu. Madhumuni ya Umoja yatakuwa ni yale tuyaliyoorodheshwa kwenye ibara ya pili ya Katiba hii ambayo yanalenga kusaidiana na kushirikiana katika masuala ya kuisaidia jamii nzima ya Watanzania hasa wale waishio katika mazingira magumu pale mfuko wa Umoja utakapokuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

**KWA KUWA** sisi waendesha pikipiki za kibiashara (Bodaboda) ni Raia halisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunalo jukumu la kuelimisha wenzetu juu ya matumizi bora ya Usalama wa Barabarani na utii wa sheria bila shuruti.

**KWA HIYO BASI**, sisi sote waendeshaji wa Pikipiki za kibiashara, wamiliki wa vyombo hivi, tunaazimia kushirikiana na wataalam na taasisi/wadau wengine wa maendeleo kwa pamoja na kuunda umoja wetu utakao hakikisha kuwa huduma ya usafiri wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu ndani ya wilaya ya Arusha mjini, inatolewa kwa kufuata sheria za nchi na kupata haki zote tunazostahili barabarani kutokana na maudhui hayo.

Katiba hii ya UBOJA ya mwaka 2017 ndio itakayoongoza utekelezaji wa shughuli za chama Ki wilaya, aidha katiba hii itaendelea kufanyiwa marekebisho na wanachama kupitia mkutano mkuu watakavyoona inafaa na kwa kuzingatia kanuni za katiba hii na sheria za Nchi. Wanachama, viongozi, maafisa na watendaji wote wa chama katika ngazi zote hawana budi kuheshimu katila hii pamoja na Sheria za Nchi.

**FASILI:**

Mahali popote ambapo maneno yanayotamkwa hapa chini yaliyotumika katika Katiba hii, yaani maana au ufafanuzi au fasiri iliyotolewa kisheria. Iwapo pana sheria yoyote nchini inayohusiana nayo, kwa maana yanakubalika na Chama**.**

**Akidi**- Ni idadi ya wajumbe wanaotakiwa ili kikao kianze.

**Alama**- Alama ni ishara ya kitu Fulani, kutakuwepo na alama katika kila Pikipiki na dereva. Itakayoonyesha ishara ya kutambua Pikipiki za Magurudumu mawili na matatu pamoja na dereva kwa kila kituo.

**Namba**- Ni idadi ya vitu, kutakuwepo na namba maalum itakayowekwa kwa kila Pikipiki za magurudumu mawil na matatu itakayonyesha idadi ya Pikipiki katika kila kituo, namba hizo zitawekwa pia katika kila vazi la Dereva**, (reflector)**

**Ajali**- ni tukio la dharura la kusababisha kutokea majeraha, maumivu ama kifo kutokana na mgongano wa vitu viwili kama gari na Pikipiki, Pikipiki na Pikipiki, Pikipiki na mwenda kwa miguu, dereva wa Pikipiki na abiria wake au dereva wa Pikipiki kuanguka pekee yake itahesabika kama hiyo ni ajali.

**Bodi ya Wadhamini** - Kutakuwa na bodi ya wajumbe Chombo cha wadhamini wa Chama chenye wajumbe watatu.

**Nembo ya Chama** - Alama ya chama itakuwa na mchoro wa barabara, pikipiki yenye magurudumu mawili na matatu.

**Fomu ya uanachama**- Fomu itakuwa na taarifa zote muhimu zinazomhusu mwanachama na chombo anacho kilimili au kukuendesha na sehemu anayopaki ( kituo chake)**.**

**Chama** -Ni Umoja wa madereva na wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu, waliosajiliwa kufanya biashara za usafirishaji wa abiria.

**UBOJA**- Umoja wa Bodaboda Jiji la Arusha - Taratibu zinazoitafsiri Katiba na kutoa mwongozo wa utekelezaji wake.

**Katiba-** Katiba ndio sheria mama za chama. Ni sheria itakayosimamia uendeshaji wa shughuli za umoja (UBOJA) Ambayo itatumika kusimamia na kuelekeza fikra, mitazamo na maono ya wanachama ili kufikia malengo na madhumuni ya uanzishwaji wa Umoja.

**Mwanachama** – Ni Dereva wa pikipiki ya magurudumu mawilli na matatu ambaye anafanya biashara ya usafirishaji wa abiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

**Uongozi**: Ni dhamana ambayo imekabidhiwa kwa baadhi ya Wanaumoja ili waongoze wanaumoja na Umoja kwa ujumla ilikufikia malengo ambayo wanaumoja wamejiwekea. Kama mme au mke, mmojawapo atachaguliwa kuwa kiongozi wa umoja, aliyechaguliwa Ndiye kiongozi na siyomwenzi wake. Ushirika unabakia kwenye uanachama na siyo majukumu aliyokabidhiwa mmoja wao kama kiongozi;

**Kiongozi** - Mwanachama yeyote aliyechaguliwa na Chama au kuajiriwa na Chama kushika nafasi yoyote ya uongozi katika Chama.

**Mwenyekiti** - Kiongozi Mkuu wa Chama katika ngazi husika.

***Mwenyekiti Msaidiz***i - Kiongozi mkuu msaidizi wa Chama katika ngazi husika**.**

**Katibu Mkuu** - Mtendaji Mkuu wa shughuli za Chama katika ngazi ya husika.

**Naibu Katibu Mkuu** - Mtendaji Mkuu Msaidizi wa Chama**.**

***Mweka Hazina*** - Mtunza Hazina wa Chama katika ngazi husika.

**Kiongozi wa Nidhamu (kamanda**) ni msimamizi mkuu wa nidhamu ndani ya chama**.**

**Mlezi:** Mtu yeyote yule mwaminifu, mkarimu, msikivu, mwenye upendo na meandeleo ya watu, atakayependekezwa na bodi ya wakurugenzi kutekeleza na kuwa Mlezi kama Mshauri wa Chama katika mambo yote yanayohusu maendeleo ya Chama.

**Mradi-** chama kinaweza kuwa na mradi wowote utakao buniwa kwa lengo la kukuingizia chama mapato.
***Mtalaamu***: Ina maana ya mfanya kazi wa hiari au wa kulipwa/Kuajiliwa mwenye ujuzi na kile alichoomba ama kuombwa kusaidia katika chama ambaye atakuwa ni mtendaji wa hiyari, katika chama kutoka katika sekta binafsi au serikali na anaweza kutoa ujuzi wake kama ushauri kwa chama bila kuvunja mashafti mengine ya Katiba hii.

***Mfanyakazi***- Mtu aliyeingia katika makubaliano au mkataba wa maandishi na mwajiri ambaye ni chama kwa kutenda kazi kwa kupewa fidia/malipo ya ajira /mshahara kwa kila juma, majuma au mwezi.

**Mgogoro** - Kuwepo hali isiyokuwa ya maelewano kati ya mwanachama na mwanachama mwenzake au kati ya kiongozi na viongozi wenzake au kati ya mwanachama na kiongozi.

**Mgomo** - Kitendo chochote kinachotendwa na wanachama ambacho kitasababisha uzorotaji wa kazi kutokana na kutoelewana kati ya mwanachama na chama au kati ya mwanachama na kiongozi.

**Mkataba wa hiari** - Makubaliano yaliyofikiwa kati ya dereva na mmliki, kuhusu haki na mazingira bora ya kazi na maslahi.

**Mwajiri-** Ni Mtu binafsi, Kampuni, Shirika, Serikali ambayo imeingia katika makubaliano/mkataba wa maandishi na dereva kwa madhumuni ya kutoa huduma kwa ujira.

**Ngazi za uwakilishi**- kutakuwepo na wawakilishi wa chama katika ngazi ya Vituo, Kata na Wilaya. Ngazi hizi zitachagua wajumbe wa kuhudhuria mkutano wa Kamati ya Utendaji wa Ki-wilaya. Ngazi ndiyo sehemu ya muundo wa chama kikatiba.

**Muundo wa Chama**- Kituo, kata, wilaya.

**Ulemavu** - Ni kukosa au kushindwa kuwa na fursa ya kushiriki katika maisha ya kawaida ya kijamii sawa na watu wengine kwa sababu za kimaumbile, kiakili au sababu za kijamii.

**Wadau**-Ni makundi washiriki wa maendeleo katika tasnia ya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

**ADA-** Ada ni kiasi cha fedha ambacho kila mwanachama anachangia kwenye mfuko mkuu wa umoja kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za umoja.

**SURA YA KWANZA:**

**UTANGULIZI 1.1**

**JINA LA CHAMA LITAJULIKANA KAMA:** Umoja wa waendesha Bodaboda Jiji la Arusha (UBOJA)

1.2 **MAKAO MAKUU YA CHAMA NA ANWANI**: Makao makuu ya chama yatakuwa Kaloleni Arusha Tanzania. Kata, katika Jiji la Arusha Anuani yake itakuwa S.L.P 3013 Arusha, TANZANIA. Simu 0621087351/0752947499, Barua pepe: Uboja100@gmail.com

1.3 **IMANI YA CHAMA**

1.3.1 Chama kinaamini kuwa (i) Binadamu wote duniani ni sawa.

(ii) Wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawil na matatu za kibiashara ndio injini na uti wa mgongo wa maendeleo ya uchumi wa taifa letu.

(iii) Nguvu ya wamiliki wa vyombo vya moto ndio chachu ya maendeleo ya taifa na ukombozi wao.

(iv) Kila mtu anastaili haki ya kufanya kazi katika mazingira yaliyo salama.

1.4 **HADHI YA CHAMA:**

1.4. Chama kitakuwa si cha Kiserikali, Kisiasa, kabila wala cha Kidini na kitatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti na madhumuni yaliyoainishwa ndani ya Katiba hii na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria nyingine za inchi.

1.4.2 Chama kitakuwa na uwezo wa kisheria wa:-

(i) Kushitaki na kushitakiwa

(ii) Kukopesha na kukopeshwa

(iii) Kuingia kwenye mikataba mbalimbali

(iv) Kumiliki mali

(v) Chama kitakuwa na haki ya kumshitaki mtu au taasisi yoyote endapo kitaona kuna uwezekano wa kuvuruga au kuhatarisha umoja huo.

(vi) Chama kitakuwa na haki ya kumshtaki mtu/taasisi yoyote endapo itagundua anaendesha mipango miovu au njama/kutoa lugha za kichochezi kwa makusudi ili kukidhoofisha chama.

1.5 **DIRA**: Dira ya chama ni kuwa chombo imara cha kutetea haki za madereva wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu ambao ni wamiliki kibiashara na kuhamasisha na kutetea haki za abiria.

1.6 **DHIMA**: Dhima ya Chama ni kuwaunganisha wanachama katika kuweka mazingira bora ya biashara na kutetea haki na maslahi na kuhakikisha wanapata elimu katika tasnia ya usafirishaji abiria

1.7 **LUGHA RASMI YA CHAMA**: Lugha rasmi katika shughuli za Chama itakuwa ni Kiswahili/Kiingereza.

1.8 **KAULI MBIU**

*BODABODA USAFIRI SALAMA/"BODABODA KAZI KAMA KAZI NYINGINE USIICHUKULIE POA*

**SURA YA PILI:**

2.0 **MADHUMUNI MAKUU YA CHAMA:**

2.1 **Madhumuni Uboja**

I. Kulinda haki, wajibu na maslahi ya dereva, mmiliki ambaye ni dereva

II. 2.1.2 Kusimamia, kuendeleza na kulinda maslahi ya Watumiaji wa Pikipiki ndani ya wilaya na watendaji wa UBOJA] katika mamlaka husika za Serikali na Umma kwa ujumla ili kuhakikisha kuwa kuna vivutio vya kutosha na mazingira mazuri ya kufanya biashara ya usafirishaji abiria kwa kutumia pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

III. 2.1.3 Kuhakikisha madereva wote wa pikipiki za abiria kibiashara wanafuata na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

IV. 2.1.4 Kuwa mdau mkubwa wa usalama barabarani katika kuhakikisha jitahada za serikal! Kupunguza au kumaliza ajali za barabarani zinakuwa na mafanikio chanya kwa kushiriki katika kutoa elimu ya usalama barabarani kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa barabara.

V. 2.1.5 Kuwakutanisha madereva wa pikipiki na madereva ambao ni wamiliki kibiashara ili kujadili maendeleo na matatizo yao katika matumizi ya Barabara na utoaji wa huduma zao na kutafuta mbinu ya kuzitatua changamoto za kisheria kwa kushirikiana na wasimaizi wa sheria.

VI. 2.1.6 Kujadili na kushauriana na wakuu wa mamlaka zinazosimainia kanuni na sheria ya matumizi ya barabara kwa niaba ya madereva wa pikipiki na madereva ambao ni wamiliki kibiashara kufuatilia haki, maslahi na haki nyingine zinazohusiana na mazingira ya utoaji wa huduma ya usafiri wa Pikipiki ndani ya Wilaya ya Arusha.

VII. 2.1.7 Kuishauri Serikali juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya utoaji wa huduma hii ya usafiri wa Pikipiki za biashara kama vile kuweka utaratibu wa maegesho, uongozi katika maengesho na serikali za mitaa.

2.1.7 Kuishauri Serikali namna iliyo bora ya kupambana na uhalifu wa kijinai kwa kutumia pikipiki.

(i) Kupokea maoni, malalamiko ya wanachama wa vikundi vya pikipiki ndani ya Wilaya na kuwasilisha maoni hayo katika ngazi husika ili kupata msaada unaohitajika.

(ii)

(iii) Kusuluhisha na kutatua malalamiko au migogoro mbalimbali ya wanachama katika vituo, ngazi ya Kata na Wilaya, kwa wawakilishi wa chama Kiwilaya pamoja na kuweka bayana makubaliano yaani mikataba kati ya waendasha Pikipiki na waajiri wao kwa wale watakaokuwa wameajiriwa kufanya kazi hiyo na watu binafsi na makundi yote katika jamii.

(iv) Kuandaa mikakati na mipango kazi itakayounganisha wadau wote kutekeleza mpango wa utoaji wa huduma bora na salama ya usafiri wa Abiria kwa njia ya Pikipiki.

(v) Kufanya utafiti na uchambuzi mbalimbali dhidi ya utoaji wa huduma ya usafiri wa pikipiki ili kuwa huduma bora na salama.

(vi) Kushauri na kutetea sera itakayolinda hadhi na heshima ya utoaji wa huduma hii ya usafirishaji kwa njia ya Pikipiki na kuhimiza huduma ya Afya ikiwa ni pamoja na kuwa Bima ya Afya.

(vii) Kuhimiza, kuwahamasisha na kuwataka waendeshaji wa vyombo hivi vya magurudumu mawili na matatu kuhudhuria mafunzo ya aina yoyote ile itakayowasaidia katika maendeleo ya shughuli zao

(viii) Kuhakikisha kuwa wasimamizi wa sheria za Barabarani na watumiaji wa usafiri wa Pikipiki wanazingatia na kutekeleza vyema sheria na kanuni za nchi.

2.1.8 Kusaidiana katika shida mbalimbali ambazo zitakuwa ndani ya uwezo wa wanaumoja.

Shida ambazo wanaumoja tutasaidiana ni pamoja na:

(a) Ugonjwa wa mwanachama, Mke pamoja na Watoto wanne (4) tu.
(b) Msiba wa mwanachama, Baba, Mama, Mke na Watoto wanne.
(c) Kusaidia watoto Yatima na wasiojiweza.
(d) Kutembelea wagonjwa hospitalini pamoja na kuchangia kutoa damu.

2.1.9 Kutengeneza mahusiano mazuri na serikali kufanya biashara ya usafirishaji ndani ya wilaya ya

Arusha mjini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Kuelimisha juu ya sheria mbalimbali za barabarani ili kuepuka ajari.

2.1.10 Kudumisha amani, umoja na mshikamano katika umoja wetu pamoja na nje ya umoja. Kuomba tenda mbalimbali katika jiji la Arusha. Kuanzisha taasisi ya mikopo kwa wana Umoja kwa ajili ya kukopeshana. Kujadiliana na taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali kwa ajili ya kuinua uwezo wa kiuchumi kwa Wanaumoja ili kupata mikopo mbalimbali kama:

(a) Pikipiki.
(b) Vipuri.
(c) Fedha.
(d) Viwanja.
(e) Nyumba. n.k.
(i) Kuhakikisha tunashirikiana na taasisi mbalimbali zitakazo kuwa tayari kushirikana na umoja ili kutoa fursa kwa wanachama wetu.
(ii) Kuanzisha vituo vipya vya waendesha bodaboda kuanzia ngazi ya kata na wilaya.
(iii) Kufuta vituo ambavyo havitambuliwi na Umoja wetu.
(iv) Kuanzisha na kuimarisha ulinzi shirikishi ili kutokomeza uhalifu.
(v) Kuandaa mawasiliano bora kati ya madereva na wamiliki ambapo dereva asiye na sifa asiajiliwe au kusajiliwa katika kituo chochote ndani ya Jiji la Arusha.
(vi) Kuimarisha usafi wa mazingira
(vii) Kuelimisha abiria juu ya haki zake za msingi kabla ya kupanda pikipiki
(viii) Kupanua wigo wa ajira kwa vijana
(ix) Kuanzisha saccos ( kuanzisha miradi mbalimbali

(ix) Kuanzisha timu za mpira na michezo mbalimbali
(x) Kuwa na mifumo wa mawasiliano kunanzia ngazi ya wilaya, kata hadi kituo.
(xi) Kuimarisha mfumo wa utambuzi wa wanaumoja ndani ya wilaya ya Arusha

**SURA YA TATU:**

**3.0 UANACHAMA;**

**3.1 UANACHAMA KWENYE UMOJA WA BODABODA WILAYA:**

3.1.1 Uanachama kwenye umoja wa bodaboda jiji la Arusha umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni:

A. wanaumoja waanzilishi waliokutana kwa mara ya kwanza na kuanzisha umoja huu

B. wanachama waliojiunga baadae

C. wanaumoja walioanzisha na waliojiunga baadae wote watajulikana kama wanachama au wanaumoja kwa mujibu wa katiba hii.

Ili mtu yeyote apokelewe kwenye umoja wa waendesha bodaboda wilaya sharti awe na sifa zifuatazo:

a. Umri wa miaka 18 au zaidi
b. Awe anafanya biashara ya kuendesha pikipiki ya magurudumu mawili au matatu ndani ya jiji la Arusha.
c. Mwaminifu
d. Mwenye akili timamu
e. Sifa nyingine ni zile zilizoainishwa kwenye kanuni za umoja wa wilaya
f. Ni kinyume cha masharti ya katiba hii kwa mtu yeyote ambaye hajasajiliwa kupitia namba ya kituo na namba ya ubavuni kuendesha pikipiki ya magurudumu mawili au matatu kujiunga na umoja huu.

Kama mwenye kuomba kuwa mwanaumoja alishakuwa mwanaumoja
a. Kabla ya kupokelewa atalipa madeni aliyoacha kabla ya kuondoka kwenye umoja
b. Kama alifukuzwa kwa kukiuka taratibu za umoja au aliacha madeni, atakuwa kwenye kipindi cha majaribio kwa mwaka mmoja
c. Mwanaumoja aliyekwenye kipindi cha majaribio hatapewa huduma yoyote.
d. Mwendesha bodaboda yeyote anaetoa huduma ya usafirishaji ndani ya jiji la Arusha lazima awe amesajiliwa ndani ya kituo/ofisi atakapofanyia kazi.
e. Taarifa zake lazima zifike ngazi ya kituo, kata, wilaya pamoja na halimashauri ya jiji la Arusha.

**3.1.1 KUJIUNGA NA UMOJA WA BODABODA JIJI LA ARUSHA (UBOJA)**

3.1.2 Taratibu za kujiunga na umoja wa bodaboda jiji la Arusha
3.1.3 Mtu mwenye kujiunga na umoja wa bodaboda atafuata taratibu zifuatazo:
a) Atakuja na barua ya utambulisho kutoka kwa afisa mtendaji wa kata
b) Mwenyekiti wa mtaa wake ikiwa imegongwa mhuri pamoja na passport size 3
c) Atajaza form inayopatikana kwa katibu wa kituo husika lakini pia baada ya kujaza form hiyo itaambatanishwa na vitu vifuatavyo:
    i. COPY YA LESENI YA UDEREVA
    ii. COPY YA LATRA
    iii. COPY YA BIMA NA STIKA YA NENDA KWA USALAMA BARABARANI
    iv. HELMET MBILI (02) NGUMU
    v. Zitakaguliwa na mwenyekiti wa kituo husika mahali ambapo unataka kupaki.

vi. Ataweka fedha ya kiingilio kwenye account ya Umoja Kama ilivyoainishwa kwenye kanuni.
vii. Atapeleka form iliyojazwa na bank slip kwa katibu wa kituo
viii. Viongozi wa kituo watajadili na kujiridhisha kuwa imejazwa ipasavyo.
ix. Katibu wa kituo ataweka maoni yake ya kituo.
x. Katibu wa kituo atapeleka form ya bank slip Kwa katibu wa kata husika na katibu wa kata husika atapeleka bank slip hiyo kwa katibu mkuu wa wilaya.

f. Baada ya kupokea form katibu mkuu wa wilaya atajiridhisha kwa taarifa zifuatazo
   i. Form imejazwa kwa ukamilifu
   ii. Taarifa zilizojazwa hazina mashaka
   iii. Mwombaji anasifa za kujiunga na umoja?
   iv. Iwapo katibu mkuu atajiridhisha kwamba form imejazwa ipasavyo ataifikisha kwenye kikao cha kamati kuu ili ijadiliwe.
g. Mtu yeyote atachukuliwa kuwa amepokelewa kwenye umoja baada ya:
   i. form yake ya maombi ya kujiunga na umoja kujadiliwa na kikao cha kamati kuu na kufikia uamuzi wa kumpokea
   ii. Mwanachama anayejiunga kwenye umoja wa Bodaboda jiji la Arusha atalipa kiingilio cha kiasi cha fedha kilichoainishwa kwenye kanuni za umoja na kukatiwa risiti ya uthibitisho wa malipo ambayo udhibitisho wake ni bank deposite slip iliyoambatanishwa kwenye form ya maombi ya kujiunga na umoja.
h. Mtu atachukuliwa kuwa mwanaumoja kuanzia tarehe ya stakabadhi ya malipo ya kiingilio.
i. Mtu yeyote ambaye form yake imekataliwa Kwa sababu ya kutoa taarifa za uongo au uanachama wake umekuwa batili Kwa sababu za uongo wakati wa kujaza form za usajili hatarudishiwa fedha alizotoa kwenye umoja.

**CHAMA KIMEWEKA UTARATIBU WA KUSAJILI WANACHAMA WAPYA NA KUFUNGUA KITUO KIPYA KAMA IFUATAVYO:**

Katiba hii ya umoja wa waendesha Bodaboda jiji la Arusha inatambua kwamba wanaoruhusiwa kusajiri wanachama wapya na kufungua vituo vipya ni:

(a) Viongozi wa bodaboda wilaya na
(b) Viongozi wa bodaboda kata.

Viongozi waliotajwa hapo juu kikatiba ndio wenye mamulaka ya kupeleka wanachama wapya kwenye vituo na kufungua vituo vipya.

Ni kinyume na utaratibu viongozi wa serikali au viongozi wa chama chochote cha siasa kujihusisha na ufunguzi wa vituo vyovyote au kupeleka mwanachama yoyote kwenye kituo.

**j. HAKI ZA MWANACHAMA AU MWANAUMOJA**

Haki za mwanaumoja:

k. Mwanachama wa bodaboda wilaya ya Arusha mjini atakuwa na haki zifuatazo:
   iii. Kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa umoja
   iv. Kupata taarifa ya mali au fedha za umoja
   v. Kupata taarifa za mapato na matumizi ya kila mwezi
   vi. Kupata taarifa juu ya mwenendo wa taarifa za shughuli za umoja

vii. Kupewa fursa ya kujitetea mbele ya kamati ya nidhamu na maadili ngazi ya kituo, kata na Wilaya.
viii. Kama matatizo ni ya uongozi mkuu wa wilaya, rufaa yake itaishia kwenye bord ya wadhamini ya chama kupitia kamati kuu na kamati ya usuluhishi.
ix. Bodi ya wadhamini wanayo mamlaka kuonya, kusimamia na kushauri kamati zote ndani ya chama wilaya, kuchukua hatua za kinidhamu kwa kiongozi yeyote Yule pale panapo shindikana , na kamati kuu italazimika kuitisha mkutano mkuu kwaajili ya kutoa mapendekezo na maamuzi ya mwisho dhidi ya kiongozi husika ngazi ya wilaya.
x. Kutetea maslahi na haki zake za chama kuhusiana na shughuli zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na katiba hii.
xi. Kushiriki na kufaidi matunda yote au mafanikio yatokanayo na ushiriki wake katika chama kwa ujumla.
xii. Kupata haki ya kukata rufaa iwapo hakupata haki kutoka kwenye kamati ya nidhamu na maadili.
xiii. Kushiriki kwenye shughuli za umoja
xiv. Kuhudumiwa wakati wa shida na raha kwa huduma zilizoainishwa kwa mujibu wa katiba hii
xv. Kutoa mawazo kwa uhuru bila kuzomewa, kutishiwa, kushurutishwa au kushawishiwa na mtu yeyote ilimradi havunji taratibu za umoja.

A. ***WAJIBU WA MWANACHAMA NDANI YA UMOJA KUANZIA WILAYA/KATA HADI KITUO:***
B. Kuchagua na kuchaguliwa, kushika nafasi ya uongozi wa chama
C. Kujitetea na kutoa maelezo mbele ya kikao cha chama au chombo kinachohusika katika mashitaka yoyote yaliyotolewa dhidi yake.
D. Kupata taarifa ya fedha na mali za umoja mara 1 kwa mwaka ngazi ya wilaya wakati wa mkutano mkuu.
E. Kupata taarifa juu ya mwenendo wa shughuli za umoja
F. Kupewa fursa ya kujitetea mbele ya kamati ya nidhamu na maadili ya kata, endapo hataridhika na maamuzi yaliyotolewa dhidi yake, atakata rufaa kwa kamati ya nidhamu na maadili ngazi ya wilaya.
G. Kila mwanachama atakuwa na haki ya kupata huduma zilizoainishwa kwa mujibu wa katiba.
H. Kutoa mawazo kwa uhuru kwenye vikao bila kuzomewa, kutishiwa, kushurutishwa ama kushawishiwa na mtu yeyote ilimradi havunji taratibu za umoja
   Mwanachama wa umoja ndani ya jiji la Arusha atakuwa na wajibu ifuatavyo:
   a. Kusoma na kuelewa katiba ya umoja
   b. Kulinda, kutetea na kuheshimu katiba
   c. Kulipa ada na michango mingine ndani ya muda uliowekwa.
   d. Kuunga mkono nakusaidia kwa maneno na vitendo maendeleo ya umoja
   e. Kuhudhuria mikutano, vikao halali vilivyowekwa kikatiba pamoja na misiba
   f. Shughuli nyingine za umoja zitakavyoamriwa na vikao vya umoja.
   g. Kuhudhuria mafunzo ama semina ya aina yoyote kadri itakavyotolewa taarifa na uongozi katika ngazi husika ili kujiendeleza ili kupata maarifa mapya
   h. Kutoa msaada kwa wenzake na kushiriki shughuli za pamoja za wanachama.
   i. Kutoa taarifa kwa uongozi kwa haraka iwezekanavyo kwa pale itakapohitajika msaada wa viongozi wa ngazi zote

j. Kutoa ushirikiano wa maswala yote yanayohusu usalama wa Nchi ikiwa ni pamoja na kushiriki mikutano mbalimbali ya maendeleo ya wananchi na viongozi wa serikali.

k. Kutokujichukulia sheria mkononi kwa pale tatizo linapotokea, na maramoja watoe taarifa kwa ngazi husika pale tatizo linapotokea

**UKOMO WA UANACHAMA:**

Sababu zinazopelekea ukomo wa mwanachama:

Uanachama wa mwanachama utakoma kwa sababu ya mambo yafuatayo.

1. Kifo
2. Kudhibitisha kwamba taarifa zilizofanya apokelewe kwenye umoja zilikuwa za uongo
3. Kufukuzwa kwa sababu mbalimbali kama vile:
    a. Kujiondoa kwa hiari yake mwenyewe kwa kuandika barua
    b. Kuondolewa au kufukuzwa uanachama na mkutano mkuu kwenye ngazi husika
    c. Kutohudhuria mikutano mi 3 kwa mfululizo bila taarifa yoyote kuanzia ngazi ya kituo, kata na Wilaya
    d. Kutokutoa ada kwa muda wa miezi mitatu mfululizo bila sababu za ugonjwa
    e. kubainika kuwa ni mwizi
    f. Ubakaji/ulawiti

**Mwanachama anaweza kufukuzwa kwenye umoja iwapo;**

a. Akikaidi kutekeleza uamuzi wa kamati ya nidhamu na maadili au uamuzi wa kamati ya rufaa kwa zaidi ya miezi mitatu.
b. Endapo akikaa bila kulipa ada ya umoja au kituo kwa muda wa miezi mitatu
c. Endapo atakataa kulipa mchango halali uliowekwa kwa mujibu wa katiba hii au kwa uamuzi wa mkutano mkuu

**Mwanachama kuadhibiwa:**

**Utoaji wa adhabu kuanzia ngazi ya kituo, kata hadi Wilaya.**

**1.** Mwanachama anaweza kuadhibiwa Kwa kutozwa faini kuanzia kituo, kata hadi wilaya Kwa viwango vilivyoainishwa kwenye kanuni iwapo atatenda makosa yaliyokatazwa Kwa mujibu wa katiba.
**2.** Mwenyekiti wa kikao au mkutano anaweza kutoza faini ya papo Kwa papo Kwa makosa yafuatayo.
    **a.** Mwanachama kuongea kwenye kikao au mkutano bila ruhusa ya mwenyekiti
    **b.** Kumzomea, kumkatiza kuongea, kutoa lugha ya kashifa au kutoa maneno yenyekufanya mtu ashindwe kutoa mawazo yake kwenye kikao au mkutano wowote.
    **c.** Kusoma gazeti, kitabu, kuchati au kuongea na simu kwenye mkutano au kikao
    **d.** Mwanachama kuongea na mwanachama mwingine kwenye kikao au mkutano

**MWENYEKITI WA KIKAO AU MKUTANO ATACHUKULIWA KUWA MTENDA KOSA IWAPO:**

**I.** Atamkatiza kuongea mjumbe au mwanachama kwa sababu ya kumpatia mwongozo

**II.** Mwenyekiti atakuwa na jambo la kueleza ili baadae amruhusu kutoa mawazo yake.

**III.** Mwanachama au mjumbe ametumia kuongea Kwa muda mrefu zaidi ya ule uliopangwa hivyo mwenyekiti amalizie Ili wengine wapate muda wa kuchangia.

**SURA YA NNE:**

**SURA YA NNE**

VIKAO VYA UMOJA NA MAJUKUMU YAKE

4.0 MKUTAMO MKUU

4.1 Mkutano mkuu utakuwa ni mkutano wa wanaumoja wote ambao ndio chombo cha juu Kabisa cha maamuzi katika umoja.

4.2 Wajumbe wa mkutano mkuu watakuwa ni viongozi wote wa vituo wa umoja.

4.3 Mkutano mkuu utafanyika mara moja kwa mwaka mwanzo wa mwezi wa 12.

4.4 Akidi ya mkutano mkuu itakuwa ni %75 ya wajumbe wote wa umoja.

4.5 mkutano mkuu wa dharura utaitishwa kwa uamuzi wa halmashauri kuu (viongozi wa kata) endapo kutakuwepo na jambo lolote la dharura linalohitaji uamuzi wa mkutano mkuu au kwa maagizo ya uongozi wa juu.

4.6 Akidi ya mkutano mkuu wa dharura itakuwa ni %40 ya wajumbe wote wa umoja.

4.7 Mkutano mkuu utaanza saa 3 asubuhi na kumalizika saa 10 jioni.

4.8 Kwa ridhaa ya wajumbe waliowengi dk 15 kabla ya muda wa kawaida wa kikao kuisha mwenyekiti wa mkutano anaweza kuongeza dakika hadi dk 30 kumalizia agenda zilizobaki

**TAARIFA ITAKAYOTUMIKA KUWAJULISHA WAJUMBE WA MKUTANO MKUU.**

4.9 Katibu mkuu wa umoja atatoa taarifa Kwa wajumbe Kwa njia ya barua au ujumbe mfupi wa maneno Kwa njia ya simu

4.10 Katibu mkuu atatoa taarifa hii ya mkutano mkuu wiki moja kabla na wajumbe wadhibitishe kupokea ujumbe huo

**MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU:**

4.11 Mkutano mkuu utakuwa na majukumu yafuatayo

a. kupokea na kujadili taarifa ya hali ya umoja ngazi ya kituo, kata hadi wilaya kwa kipindi cha mwaka mmoja
b. kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka mmoja
c. kupokea taarifa ya kiutendaji ndani ya mwaka mmoja

d. Kutoa maelekezo, madaraka Kwa halimashauri na kamati kuu Kwa maswala mahususi kadri utakavyoona inafaa ilimradi isiwe kinyume ya katiba ya umoja.
e. Wajumbe watakaochagua viongozi ngazi ya wilaya ni wajumbe wa mkutano mkuu
f. Kupitisha marekebisho ya katiba ya umoja
g. Viiongozi waliochaguliwa ( au uongozi mzima) wanaweza kuondolewa madarakani kabla ya kutimiza miaka (5) iwapo itatokea theluthi ¾) ya wanachama wote wa wilaya ya Arusha watadai kwa maandishi na kutia saini zao kuitishwa kwa mkutano mkuu maalum kwa sababu ya upungufu wa kiongozi/makosa ( au uongozi mzima) na katibu mara tu atakapopata madai hayo, atatoa taarifa ndani ya siku kumi na nne (14) ya kuitisha mkutano mkuu maalumu ambao utajadili hoja za wanachama walioitisha mkutano huo na hawezi kuendelea na madaraka yake, basi ataondolewa na mkutano huo na nafasi yake itajazwa na mkutano huo. Ila tu kiongozi hataondolewa madarakani bila kupewa fursa ya kujitetea.

**HALMASHAURI;**

4.12 **Halmashauri ya Umoja,**

4.13 Halmashauri ni chombo ambacho kitapokea mapendekezo yaliyojadiliwa na kamati kuu

4.14 Kwa minajili ya uwajibikaji wa pamoja (Collective responsibility) na uhifadhi wa siri za vikao/wajumbe wa halmashauri wanawajibika kulinda na kutetea maamuzi yaliyofikiwa hata Kama kuna mjumbe asiyeunga mkono maamuzi hayo ilimradi maamuzi wanayoyatetea

a. siyo kinyume cha katiba hii
b. hayalengi kuzuia haki kutendeka
c. hayakiuki misingi ya umoja na mshikamano katika umoja
d. hayana misingi ya ubaguzi

**VIKAO VYA HALMASHAURI;**

4.15 Wajumbe wa kikao cha halmashauri kuu watakuwa ni viongozi wote wa kamati kuu, viongozi wa kata na wenyeviti wa kamati mbalimbali za kikatiba

4.16 kikao cha halmashauri kuu kitakaa mara mbili Kwa mwaka.

4.17 Halmashauri inaweza kukaa vikao vya dharura wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo kwa maagizo ya uongozi wa juu.

4.18 Kikao kitafanyika mwanzo wa mwezi wa sita (6) na mwanzo wa mwezi wa kumi na moja (11)

**MAJUKUMU YA HALMASHAURI**

4.19 Halmashauri ya Umoja itakuwa na majukumu yafuatayo:

a. kupokea na kujadili taarifa ya kamati kuu juu ya hali ya umoja/kata/vituo na kamati za kikatiba
b. kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka
c. Kutunga kanuni na taratibu na sera zote za chama.
d. Kutekeleza maamuzi yatakayotolewa na Mkutano Mkuu na pia ushauri utakaotolewa na Bodi ya Wadhamini au Mlezi au Walezi wa chama
e. Kuunda Idara za Taasisi kutegemeana na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali mahsusi za chama kama idara ya (Mipango na fedha, sheria na usalama barabarani, Elimu, michezo na burudani,

Uchaguzi, Nidhamu na idara nyingine kutokana na mahitaji ya taasisi) kamati itaandaa kanuni na wajumbe wa kamati zote zitakazo ainishwa

f. Kupitisha na kupendekeza mambo na taarifa mbalimbali zinazohusu hali na ustawi wa usalama barabarani ndani ya wilaya ya Arusha mjini.
g. Kutoa muhtasari wa shughuli zote na maamuzi/majukumu yaliyopaswa kutekelezwa mbele ya kamati kuu
h. Kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali mbalimbali za chama. Kupendekeza jina la mkaguzi wa mahesabu na kuliwasilisha mbele ya wajumbe Mkutano Mkuu wa chama ili kuidhinishwa.
i. Kumsimamisha kiongozi yeyote mwakilishi au mwanachama yeyote anayetuhumiwa kukiuka Katiba na maadili ya chama na baada ya kupitia kwa kina tuhuma hizo na kumpa mtuhumiwa haki ya kusikilizwa na kuwasilisha mapendekezo mbele ya Mkutano Mkuu ama umfukuze uongozi au imrejeshee uongozi mtuhumiwa
j. Kujadili maswala ya jumla yatakayozingatiwa na kamati kuu wakati wa kuandaa taarifa itakayowasilishwa na kamati kuu kwenye mkutano mkuu.
k. Kujadili na kupitisha kanuni mbalimbali za umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa katiba

**KAMATI KUU YA UMOJA YA WILAYA:**

**4.20** Kamati kuu Ni chombo cha utekelezaji wa maswala yote yatakayopitishwa na halmashauri kuu na mkutano mkuu wa umoja.

**VIKAO VYA KAMATI KUU**

**4.21 Error! Bookmark not defined.MAJUKUMU YA KAMATI KUU**

4.22 Kamati kuu itakuwa na majukumu yafuatayo

a. Kuhakikisha kunakuwepo umoja na mshikamano kwenye umoja.
b. Kusimamia maendeleo na kutoa miongozo ya utendaji kwenye kata, vituo na kamati za kikatiba
c. Kusimamia utekelezaji wa kanuni, katiba na kuhakikisha ustawi wa umoja kwa ujumla.
d. Kuratibu shughuli za kila siku za umoja.
e. Kupokea wanachama wapya wanaojiunga na umoja.
f. Kusimamia mapato na matumizi kwenye kata na vituo.
g. Kusimamia nidhamu kwa wanachama katika utaratibu tuliojiwekea.
h. Kuhamasisha ulipaji wa ada na michango mbalimbali kwa wanachama.
i. Kutoa taarifa kwa wanachama ilimradi taarifa hizo haziathiri malengo na madhumuni ya umoja.
j. Kufuatilia masuala, maamuzi na maandalizi yanayopaswa kufanywa kwa ajili ya chama katika sehemu mbalimbali ikiwemo serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi zingine.
k. Kumwongezea majukumu madogomadogo kiongozi yeyote kwa jinsi itakavyoona inafaa ili akaimu nafasi ya kiongozi ambayo iko wazi au mwenye kuishikilia anaudhuru unaomfanya asiweze kutekeleza majukumu yake. Baada ya kumwongezea majukumu kiongozi kamati kuu itawajulisha wanachama eidha kupitia viongozi wa kata au mkutano mkuu.
l. Kwa kushirikiana na kamati ya fedha na uchumi
    1. Kubuni na kuibua fursa mbalimbali za maendeleo ya umoja ikiwa ni pamoja na: miradi.
    2. Kutathimini maendeleo ya umoja kiuchumi

3. Kuchukua hatua kwa nia ya kujikwamua au kujitegemea kiuchumi

m. Kwa kushirikiana na kamati ya nidhamu na maadili:
    1. Kushughulikia maswala yanayohusiana na nidhamu kwa wanachama
    2. Kusimamia uwajibikaji kwenye umoja
    3. Kusimamia viongozi wa kata na vituo
    4. Kusimamia viongozi wa kikatiba

n. Kupanga na kusimamia shughuli zote za chama za kiutawala na pia shughuli zote za kamati ndogo za chama

o. Kupanga kalenda ya vikao vyote vya chama ikiwa ni pamoja na vikao vya

a. Mkutano Mkuu wa chama
b. Bodi ya Wadhamini
c. Kamati Kuu
d. Halmashauri kuu
e. Mikutano mingineyo kama itakavyoonekana inafaa

**KAMATI ZA KIKATIBA**

4.23 Kamati za kikatiba

4.24 Kutakuwepo na kamati za kikatiba ambazo ni
- (i) Kamati ya uchaguzi
- (ii) Kamati ya fedha na uchumi/mipango
- (iii) Kamati ya nidhamu na maadili
- (iv) Kamati maalum

**( I ) KAMATI YA UCHAGUZI:**

**MAJUKUMU YA KAMATI YA UCHAGUZI;**

4.25 Kamati hii ya uchaguzi itaratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi ngazi ya wilaya na kata.

4.26 kamati hii itaongozwa na mwenyekiti atakayechaguliwa na wajumbe wa kamati

4.27 Wajumbe wa kamati watamchagua makamu mwenyekiti wa kamati, wajumbe wengine watakuwa wajume

4.28 Katibu wa kamati na msaidizi wake watateuliwa na kamati kuu miongoni mwa makatibu wa kata

**(II) KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

4.29 kamati ya fedha na uchumi itakuwa na majukumu yafuatayo:
- a. kuibua miradi mbalimbali ya chama
- b. kutathimini maendeleo ya chama kifedha na kiuchumi
- c. kushauri chama juu ya hatua za kuchukua kwa nia ya kujikwamua na kujitegemea kiuchumi
- d. kuishauri kamati kuu kwa maswala yanayohusu fedha na michango, na
- e. majukumu mengine watakayopangiwa na kamati kuu/halmashauri au mkutano mkuu

**(III) KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI:**

4.30 kamati ya nidhamu na maadili itakuwa na majukumu yafuatayo:

a. kushughulikia maswala yote ya nidhamu yatakayoletwa na katibu mkuu wa chama
b. kuelekeza hatua za kuchukua dhidi ya kata, kituo, kamati au mwana umoja aliyekutwa na hatia ya kukiuka taratibu za chama
c. kuuchauri umoja/chama juu ya maswala yanayohusiana na nidhamu na maadili
d. kushughulikia makosa yote isipokuwa makosa ya jinai

4.31 katika kushughulikia maswala ya nidhamu:

- kamati itamwalika mwanachama/kumjulisha na kumfafanulia tuhuma dhidi yake
- kamati itampatia nafasi mwanachama kujitetea dhidi ya tuhuma inayomkabili
- kamati itachambua utetezi dhidi ya makosa ya mwanachama anayotuhumiwa nayo
- kamati ya nidhamu itaandika uamuzi ambao pande zinazohusika na shauri hilo zitapewa uamuzi na nakala kwa katibu mkuu wa chama, katibu wa kata na katibu wa kituo anachotokea mlalamikiwa/mlalamikaji
- Kamati itatoa uamuzi wa haki/ wenye kuzingatia misingi/mila na desturi za utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za nchi.

4.32 kamati ya nidhamu na maadili haitakuwa na mamlaka ya:

a. kushughulikia shauri lolote isipokuwa lile litakalofikishwa mbele yake na katibu mkuu wa chama, na
b. katibu mkuu ndiye mlalamikaji katika mashauri yote

**(IV) KAMATI MAALUMU:**

4.33 Kamati maalumu inaweza kuundwa na halmashauri au mkutano mkuu baada ya wajumbe wake kupendekezwa na kamati kuu

4.34 Kamati maalumu:

a. Itaundwa iwapo kuna jambo maalumu linalohitaji uchunguzi wa kina
b. Ikiundwa wajumbe wake watatangazwa aidha kwenye mkutano mkuu au vikao vya kata ili wanachama wote wajue
c. Kazi za kamati/habibu za rejea zitajulikana kwa wanachama wote.
d. Mamlaka ya uteuzi ambayo ni kamati kuu ndiyo itakayoamua kuiteua viongozi wa kamati hiyo
e. Taarifa ya matokeo ya kazi itakayo fanywa na mamlaka husika itawasilishwa kwa mamlaka iliyoiunda
f. Taarifa ya kamati maalumu itawekwa wazi kwa wanachama wote kupitia mkutano mkuu au kata na vituo
g. Uhai na kazi ya kamati maalumu utaisha baada ya kukabidhi taarifa kwa mamlaka iliyoiunda

**UONGOZI WA BODABODA KATA;**

4.35 muundo wa bodaboda kata, ndicho kitovu na kielelelezo cha umoja/na mshikamano wa wanachama wa (UBOJA) kwa hiyo muundo wa uongozi wa bodaboda kata siyo kikundi kinachojitegemea kwenye umoja, hivyo:

a. muundo wa bodaboda ngazi ya kata ni sehemu ya umoja
b. muundo wa bodaboda kata hautakuwa na maslahi ambayo yanaashilia kutofautiana na Wilaya au na kata zingine
c. muundo huo huo utafanya mambo yaliyoelekezwa na katiba hii tu
d. iwapo uongozi wa kata unataka kuanzisha jambo lolote lazima uombe idhini kwa uongozi wa Wilaya kwa maandishi, na wilaya iridhie kwa kuwajibu kwa maandishi
e. Viongozi wa kata wanawajibika kusimamia utii wa katiba na maelekezo ya mamlaka za juu kwenye chama.
f. Wanachama wa umoja lazima wawe chini ya uongozi wa kata na kuendelea kufanya kazi ndani ya kata kwamaelekezo waliyopangiwa na kamati kuu
g. Utata wowote utakao husu mipaka ya kata kwa kata, kamati kuu itawajibika kutoa uamuzi wa utata huo na uamuzi wa kamati kuu ndio utakuwa uamuzi wa mwisho

**4.36**

**4.37 KUHAMA KWA MWANACHAMA:**

Mwanachama atakayehamia eneo la kata nyingine ili kufanya kazi, lazima ajaze form ya eneo analo hamia. Mwanachama atakaye kiuka masharti ya kifungu hiki:

a. Atafikishwa mbele ya kamati ya nidhamu na maadili kwa kufanya kazi nje ya mipaka ya eneo lake la kazi kwa zaidi ya siku 30 bila kujaza form ya kuhama kata.
b. Hatapewa huduma yoyote ya umoja kwa tukio litakalomkuta akifanyia kazi nje ya kata aliyopangiwa kwa zaidi ya siku 30
c. Katibu mkuu atawajibika kutoa maelekezo ya kimaandishi kwa kata aliyopangiwa ili kumfuta kutoka kwenye orodha ya wanachama wa kata aliyotoka
d. Mwanachama huyo atawajibika kulipa faini kwa kutohudhuria vikao vya kata, na
e. Atakuwa siyo mwanachama hai tangia tarehe ya kufutwa toka kwenye daftari la wanachama aliopangiwa.
f. Endapo mwanachama huyo ataomba msamaha kwa maandishi ndani ya kata husika, na kupeleka nakala kwenye uongozi wa wilaya, baada ya kujiridhisha, katibu mkuu atawakilisha barua hiyo kwa kamati ya nidhamu na maadilii ili ajadiliwe.

**VIKAO VYA BODABODA KATA:**

4.37 Kutakuwa na vikao vya bodaboda kata vya kikatiba kama ifuatavyo:

a. Kamati kuu ya kata (viongozi wote wa kuchaguliwa)
b. Halmashauri kuu ya kata ( itakuwa ni viongozi wote wa vituo ndani ya kata)
c. Mkutano mkuu wa kata ( watakuwa ni bodaboda wote wa vituo ndani ya kata)

**KAMATI KUU YA KATA**

Kamati kuu ya kata itakutana kila baada ya Miezi mitatu, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.

**HALMASHAURI KUU YA KATA**

Halmashauri kuu ya kata itakuwa na vikao viwili kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo

**MKUTANO MKUU WA KATA**

Mkutano mkuu wa kata utafanyika mara moja kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.

**MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA KATA:**

4.38 Kata itakuwa na majukumu yafuatayo:

a. Kuwa kiunganishi cha wanaumoja walioko kwenye vituo na wale wa umoja mkubwa, kwa kuhimiza mahudhurio katika vikao mbalimbali vya umoja
b. Kuhimiza ulipaji wa michango mbalimbali na ada za umoja
c. Kuainisha kero mbalimbali katika umoja na wanaumoja hasa kuhusiana na mwenendo wa uendeshaji na usimamizi wa maswala ya umoja
d. Kutafakari juu ya uongozi wa umoja ndani ya vituo kwenye kata husika ili kama kuna maoni ya kuboresha yawakilishwe kwa katibu mkuu wa umoja ngazi ya Wilaya kwa maandishi
e. Kutambua wanachama wapya walioingia kwenye vituo ndani ya kata husika
f. Kwa kushirikiana na kamati kuu ya wilaya, kusimamia nidhamu ya wanaumoja kwenye kata husika
g. Kuhimiza wanaumoja kwenye kata kwa mujibu wa katiba hii, kuhudhuria vikao vya umoja na matukio mbalimbali ya umoja ikiwa ni pamoja na matukio ya kiserikali na taasisi nyingine.
h. Kuhakikisha kuwa wanachama walioko kwenye kata hawafanyi jambo lolote linalopingana na katiba, kanuni, maamuzi na maelekezo ya kamati kuu, halmashauri kuu, mkutano mkuu au viongozi wakuu wa umoja.

**MAJUKUMU YA HALMASHAURI KUU YA KATA:**

4.39 Halmashauri kuu ya kata ni chombo ambacho kitapokea mapendekezo yaliyojadiliwa na kamati kuu ya kata kwa minajili ya uwajibikaji wa pamoja ( collective responsibility) na uhifadhi wa siri za vikao/wajumbe wa halmashauri wanawajibika kulinda na kutetea maamuzi yaliyofikiwa hata kama kuna mjumbe asiyeunga mkono maamuzi hayo ilimradi maamuzi wanayoyatetea:

a. siyo kinyume cha katiba hii
b. hayalengi kuzuia haki kutendeka
c. hayakiuki misingi ya umoja na mshikamano katika umoja
d. hayana misingi ya ubaguzi

**MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA KATA:**

4.40 Mkutano mkuu wa kata ni chombo cha maamuzi ya mwisho ngazi ya kata

Majukumu ya mkutano mkuu ni kama ifuatavyo:

kupokea na kujadili taarifa ya kamati kuu juu ya hali ya umoja vituo na kamati za kikatiba

a. kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka
b. Kutunga kanuni na taratibu na sera zote za chama ngazi ya kata.
c. Kupitisha na kupendekeza mambo na taarifa mbalimbali zinazohusu hali na ustawi wa usalama barabarani ndani ya wilaya ya Arusha mjini.
d. Kutoa muhtasari wa shughuli zote ndani ya kata na maamuzi/majukumu, kuletwa ngazi ya wilaya.
e. Kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali mbalimbali za chama.
f. Kumsimamisha kiongozi yeyote mwakilishi au mwanachama yeyote anayetuhumiwa kukiuka Katiba na maadili ya chama na baada ya kupitia kwa kina tuhuma hizo na kumpa mtuhumiwa haki ya kusikilizwa na kuwasilisha mapendekezo mbele ya Mkutano Mkuu ama umfukuze uongozi au imrejeshee uongozi mtuhumiwa
g. Kujadili maswala ya jumla yatakayozingatiwa na kamati kuu wakati wa kuandaa taarifa itakayowasilishwa na kamati kuu kwenye mkutano mkuu.
h. Kujadili na kupitisha kanuni mbalimbali za umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa katiba

**4.41 VIKAO VYA BODABODA NGAZI YA VITUO:**

- Viongozi wa vituo watafanya vikao vinne kwa mwaka

**4.42 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA VITUO:**

a. Viongozi wa vituo watawajibika kuitisha vikao kwa wanachama wao ili kuwapatia mrejesho na miongozo ya kikatiba kutoka kwenye vikao vya kata na Wilaya.
b. Viongozi wa vituo watawajibika kukusanya michango ya kikatiba kwa wanachama wao
c. Viongozi wa vituo wanawajibika kusimamia amani kwa wanachama wao ndani ya vituo vyao
d. Viongozi wa vituo wanawajibika kujua taarifa za kila mwanachama kwenye vituo vyao ikiwa ni pamoja na
    - Barua ya utambulisho kutoka kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa eneo analotokea
    - Kuwa na leseni ya udereva
    - Awe na akili timamu
    - Awe na umri usiopungua miaka 18 na kuendelea
    - Awe na afya bora na asiwe anatumia kilevi chochote kama pombe, bangi, mirungi, sigara, pindi awapo eneo la kazi.

- Taarifa za mwanachama mpya ziende ngazi ya kituo anachoenda kufanyia kazi , kata kilipo kituo, kisha wilaya na endapo itabainika mwanachama mpya ameingia bila taarifa kupita ngazi ya kata ama wilaya uongozi wa kituo husika utawajibika.
- Kudhibiti kelele za exosit ( Tramper) na taa zenye mwanga mkali (Sport light)
- Ni marufuku mwanachama yeyote ndani ya kituo kuharibu mfumo wowote wa pikipiki, kuitoa kutoka kwenye uhalisia wake na kuibadirisha anavyotaka yeye.
- Kuhakikisha kuwa mwanachama hatoi lugha za matusi kwa abiria, mwanachama mwenzake au kwa majirani walio karibu na kituo

e. Ni marufuku kwa kituo chochote kupokea fedha mkononi za mwanachama mpya/faini na michango yoyote inayotambulika kikatiba

f. Ni lazima kila kituo kuwa na akaunti ya benki

g. Ni lazima wanachama wasomewe taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu kwenye kituo husika

h. Ni marufuku kwa mwanachama kuendesha pikipiki akiwa hana helmet (kofia ngumu) na kiaksi mwanga (reflector) chenye namba ya uanachama wake.

i. Ni lazima mwendesha bodaboda kuwa msafi wa mwili, mavazi, chombo anachoendesha, mazingira anakofanyia kazi

j. Ni lazima wanachama kushiriki shughuli mbalimbali za kiserikali na za kijamii pale itakapohitajika kufanya hivyo.

## SURA YA TANO:

### 5.0 MUUNDO WA UONGOZI;

5.1.1 Kutakuwa na muundo wa uongozi wa chama Wilaya ambao utakuwa na wajibu wa kuelekeza shughuli za kila siku chini ya usimamizi wa kamati kuu. Muundo huo utakuwa Kama ifuatavyo:

a. Viongozi wa Wilaya.

b. Viongozi wa kata.

c. Viongozi wa vituo.

5.1.2 **VIONGOZI WA WILAYA/KAMATI KUU:**

5.1.3 Viongozi wa wilaya watakuwa ni:

- Mwenyekiti.
- Makamu mwenyekiti.
- Katibu Mkuu.
- Naibu katibu Mkuu.
- Mhasibu/au mweka hazina.
- Kiongozi wa Nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu.
- Naibu msimamizi wa nidhamu.
- Afisa habari wa chama.

**5.1.4 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA UMOJA NGAZI YA WILAYA**

**5.1.5 KAZI ZA MWENYEKITI:**

a. Mwenyekiti ndiye kiongozi mkuu wa chama
b. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi wengine waandamizi
c. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu mkuu
d. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mkutano mkuu/halmashauri na kamati kuu
e. Pamoja na katibu mkuu kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya chama
f. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi
g. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali
h. Mwenyekiti wa umoja amepewa mamlaka kwa mujibu wa katiba hii ya kumusimamisha kiongozi yoyote wa kata na wa kituo anayetuhumiwa kwa kutenda makosa kinyume na katiba hii mpaka pale utakapopatikana ufumbuzi wa makosa hayo.
i. Mwenyekiti ana mamlaka ya kuteua kiongozi mwingine atakayeshika nafasi hiyo kwa muda mpaka shauri la huyo kiongozi aliyesimamishwa kupisha uchunguzi litakapopatiwa ufumbuzi.

**5.1.6 KAZI ZA MAKAMU MWENYEKITI:**

5.1.7 Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti Kama:

a. Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri /kuugua au sababu nyingine na
b. Mwenyekiti amejiuzulu au kufukuzwa uongozi

**5.1.8 KAZI ZA KATIBU MKUU:**

Katibu mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo:

a. Atakuwa ni mtendani na mratibu wa shughuli zote za umoja
b. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu, halmashauri na kamati kuu
c. Kuitisha vikao vya umoja baada ya kushauriana na mwenyekiti
d. Kuandika na kusoma mihtasari ya vikao vyote vya umoja
e. Kuweka kumbukumbu zote za umoja
f. Kufatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja
g. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja kuanzia ngazi ya kata, kamati na umoja kwa ujumla na pamoja na mwenyekiti kutia sahihi katika kumbukumbu zote za mikutano ya umoja.
h. Katibu mkuu kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri kamati kuu, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo/maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura, katibu mkuu atayawasilisha mbele ya kamati kuu ili yapate Baraka zake.

**5.1.9 MAKUJUKUMU YA NAIBU KATIBU:**

Naibu katibu mkuu ni saidizi wa katibu mkuu ambaye atafanya kazi zote za katibu mkuu kama katibu mkuu hayupo au kazi zote atakazoelekezwa kufanya na katibu mkuu au mwenyekiti au makamu mwenyekiti.

**5.1.10 MAJUKUMU YA MTUNZA HAZINA NGAZI YA WILAYA:**

Mtunza hazina atakuwa na majukumu yafuatayo:

a. Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja
b. Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama.
c. Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanaumoja ya kila mwezi
d. Kuwasilisha taarifa zote za fedha kwa kamati kuu, halmashauri kuu na mkutano mkuu
e. Kutoa na nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati kuu, halmashauri kuu na mkutano mkuu.
f. Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka kwa wanachama wote au taasisi yoyote itakayotoa fedha zipelekwe banki.
g. Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi
h. Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja (chama)
i. Kuboresha taratibu za ulipaji wa fedha kwa wanachama ili kuepuka usumbufu wa huduma.
j. Kuboresha na kusimamia taratibu za kutoa mikopo na marejesho yake
k. Bila kuathiri masharti ya katiba hii, kuidhinisha kiasi cha mchango kitakachotozwa na kata kama ada ya kata.
l. Kwa kushirikiana na kamati ya uchumi na fedha, atabuni njia mbalimbali za kuongeza mapato ya chama.

**5.1.11 MAJUKUMU YA KIONGOZI MKUU WA NIDHAMU WILAYA:**

a. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi mkuu wa maswala yote ya nidhamu ndani ya chama
b. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama katika jiji la Arusha
c. Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayotokea ndani ya chama
d. Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote
e. Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za chama zinakuwa salama kwenye vikao
f. Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya chama na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu ambazo zilizopo ndani ya katiba hii
g. Kiongozi mkuu wa nidhamu kwa kushirikiana na kamati za nidhamu na maadili atahusika kupeleka wanachama wapya kwenye vituo kwa maelekezo toka kwa mwenyekiti na katibu.

**5.1.12 MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA CHAMA NGAZI YA WILAYA:**

1. Atashirikiana na mtunza nidhamu mkuu katika utendaji wake wa kila siku
2. Atamwakilisha nidhamu mkuu endapo kama nidhamu mkuu hatakuwepo

**5.1.13 AFISA HABARI WA CHAMA;**

Kutakuwa na afisa habari wa chama

**5.1.14 MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA:**

a. Atakuwa ndiye mtoa taarifa zote za chama kwa maelekezo ya vikao vya kamati kuu

**5.1.15 MUUNDO WA UONGOZI NGAZI YA KATA:**

Viongozi wa kata watakuwa ni:

- Mwenyekiti
- Makamu mwenyekiti
- Katibu
- Naibu katibu
- Mhasibu/au mweka hazina
- Kiongozi wa mkuu nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
- Naibu msimamizi wa nidhamu

**5.1.16 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA UMOJA NGAZI YA KATA:**

**5.1.17 KAZI ZA MWENYEKITI KATA:**

j. Mwenyekiti ndiye kiongozi wa chama ngazi ya kata
k. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi wengine waandamizi
l. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu wake
m. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mkutano /halmashauri na kamati ya kata
n. Pamoja na katibu wake kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya chama ngazi ya kata
o. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi yote ngazi ya kata
p. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali ngazi ya kata

**5.1.18 KAZI ZA MAKAMU MWENYE KITI KATA:**

Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti Kama:

c. Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri /kuugua au sababu nyingine na
d. Mwenyekiti amejiuzulu au kufukuzwa uongozi

**5.1.19 MAJUKUMU YA KATIBU NGAZI YA KATA:**

Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Atakuwa ni mtendaji na mratibu wa shughuli zote za umoja ngazi ya kata
j. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu wa kata, halmashauri na kamati kuu ya kata
k. Kuitisha vikao vya umoja baada ya kushauriana na mwenyekiti
l. Kuandika na kusoma mihtasari ya vikao vyote vya umoja ngazi ya kata
m. Kuweka kumbukumbu zote za umoja ngazi ya kata
n. Kufatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja ngazi ya kata
o. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja kuanzia ngazi ya kata, vituo, kamati na umoja kwa ujumla na pamoja na mwenyekiti kutia sahihi katika kumbukumbu zote za mikutano ya umoja ngazi ya kata.
p. Katibu Kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri kamati ya kata, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo/maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura, katibu wa kata atayawasilisha mbele ya kamati ya kata ili yapate Baraka zake.

### 5.1.20 MAKUJUKUMU YA NAIBU KATIBU NGAZI YA KATA:

Naibu katibu ni msaidizi wa katibu wa umoja wa kata ambaye atafanya kazi zote za katibu mkuu wake mkuu hayupo au kazi zote atakazoelekezwa kufanya na katibu mkuu wake au mwenyekiti au makamu mwenyekiti kata.

### 5.1.21 MAJUKUMU YA MTUNZA HAZINA NGAZI YA KATA:

Mtunza hazina atakuwa na majukumu yafuatayo:

m. Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja ngazi ya kata
n. Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama ngazi ya kata.
o. Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanaumoja ya kila mwezi
p. Kuwasilisha taarifa zote za fedha kwa kamati kuu, halmashauri kuu na mkutano mkuu wa kata
q. Kutoa na nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati kuu ya kata, halmashauri kuu na mkutano mkuu wa kata.
r. Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka Kwa wanachama wote au taasisi yoyote itakayotoa fedha zipelekwe banki.
s. Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi
t. Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja (chama) ngazi ya kata
u. Kuboresha taratibu za ulipaji wa fedha kwa wanachama ili kuepuka usumbufu wa huduma.
v. Kuboresha na kusimamia taratibu za kutoa mikopo na marejesho yake
w. Kwa kushirikiana na kamati ya uchumi na fedha, atabuni njia mbalimbali za kuongeza mapato ya chama ngazi ya kata

### 5.1.22 MAJUKUMU YA KIONGOZI MKUU WA NIDHAMU KATA:

h. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi mkuu wa maswala yote ya nidhamu ndani ya chama ngazi ya kata
i. Kiongozi wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama katika kata husika.
j. Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayotokea ndani ya chama katika kata husika
k. Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote katika kata.
l. Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za chama zinakuwa salama kwenye vikao vyote vya kata.
m. Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya chama na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu ambazo zilizopo ndani ya katiba hii
n. Kiongozi wa nidhamu kwa kushirikiana na kamati za nidhamu na maadili atahusika kupeleka. Wanachama wapya kwenye vituo Kwa maelekezo toka kwa mwenyekiti na katibungazi ya kata.

**5.1.23 MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA CHAMA NGAZI YA KATA:**

3. Atashirikiana na mtunza nidhamu mkuu wake katika utendaji wake wa kila siku.
4. Atamwakilisha nidhamu mkuu wa kata endapo kama nidhamu mkuu wa kata hatakuwepo

**5.1.24 MUUNDO WA UONGOZI NGAZI YA KITUO:**

Viongozi wa kata watakuwa ni:

- Mwenyekiti
- Makamu mwenyekiti
- Katibu
- Naibu katibu
- Mhasibu/au mweka hazina
- Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
- Naibu msimamizi wa nidhamu

**5.1.25 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA UMOJA NGAZI YA KITUO:**

**KAZI ZA MWENYEKITI NGAZI YA KITUO:**

q. Mwenyekiti ndiye kiongozi wa chama ngazi ya kituo
r. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi wengine waandamizi
s. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu wake
t. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mkutano na kamati ya kituo
u. Pamoja na katibu wake kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya kituo
v. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi yote ngazi ya kituo
w. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali ngazi ya kituo

**KAZI ZA MAKAMU MWENYEKITI WA KITUO:**

Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti kama:

a. Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri /kuugua au sababu nyingine na
b. Mwenyekiti amejiuzulu au kufukuzwa uongozi

**MAJUKUMU YA KATIBU NGAZI YA KITUO:**

Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo:

a. Atakuwa ni mtendaji na mratibu wa shughuli zote za umoja ngazi ya kituo
b. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu wa kituo.
c. Kuitisha vikao vya umoja baada ya kushauriana na mwenyekiti wa kituo
d. Kuandika na kusoma mihtasari ya vikao vyote vya umoja ngazi ya kituo
e. Kuweka kumbukumbu zote za umoja ngazi ya kituo
f. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja ngazi ya kituo
g. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja
h. Katibu Kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri kamati ya kata, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo/maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura, katibu wa kituo atayawasilisha mbele ya kamati ya kituo ili yapate Baraka zake.

**MAKUJUKUMU YA NAIBU KATIBU NGAZI YA KITUO:**

Naibu katibu Ni msaidizi wa katibu wa umoja ngazi ya kituo ambaye atafanya kazi zote za katibu mkuu wake hayupo au kazi zote atakazoelekezwa kufanya na katibu mkuu wake au mwenyekiti au makamu mwenyekiti wa kituo.

**MAJUKUMU YA MTUNZA HAZINA NGAZI YA KITUO:**

Mtunza hazina atakuwa na majukumu yafuatayo:

a. Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja ngazi ya kituo
b. Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama ngazi ya kituo.
c. Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanachama
d. Kutoa nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati ya kituo.
e. Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka kwa wanachama wote fedha hizo zipelekwe banki.
f. Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi
g. Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja (chama) ngazi ya kata

**MAJUKUMU YA KIONGOZI MKUU WA NIDHAMU WA KITUO:**

a. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi mkuu wa maswala yote ya nidhamu ndani ya chama ngazi ya kituo
b. Kiongozi wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama katika kituo husika
c. Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayotokea kituo husika
d. Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote vya kituo.

e. Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za wanachama zinakuwa salama kwenye vikao vyote vya kituo.
f. Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya kituo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu ambazo zilizopo ndani ya katiba hii

**MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA CHAMA NGAZI YA KITUO :**

1. Atashirikiana na mtunza nidhamu mkuu wake katika utendaji wake wa kila siku
2. Atamwakilisha nidhamu mkuu wa kituo endapo kama nidhamu mkuu wa kituo hatakuwepo

**SURA YA SITA:**

6.01 **SIFA ZA KUWA KIONGOZI:**

6.1.1 Sifa za kiongozi huweza kuwa na tafsiri mbalimbali, lakini Kwa malengo ya ibara hii sifa za kiongozi maanayake ni:

a. Kuzungumuza na kujadiliana na watu
b. Kueleza, kushawishi na kutoa ushauri unaojenga
c. Kufanya kazi kwa vitendo ili kufikia malengo yanayotarajiwa
d. Kuchukua wajibu kwaajili ya chama na kutoa mwelekeo, maelekezo na mpangilio
e. Kutia moyo watu wengine ili kufikia malengo
f. Kuwawezecha wale waliochini yake ili kutekeleza malengo yaliyowekwa na

6.1.2 Kwa hiyo mafanikio ya umoja yatategemea uongozi bora uliopo, ili aweze kuongoza vizuri kiongozi

Inabidi:

a. Awe mtu wa kutegemewa katika maamuzi
b. Awe mwenye msimamo (asiye yumba yumba)
c. Awe mwenye uwezo wa kujenga na kusimamia hoja sahihi kwa ujasiri na kwa kujiamini
d. Awe mwadilifu katika mwenendo wake katika maisha kwa ujumla
e. Awe mwenye kujiamini katika eneo lake la majukumu na mwenye kujitoa kikamilifu katikka utendaji
f. Awe mwenye kuweza kufanya maamuzi ndani ya muda, kwa wakati mwafaka na kuyasimamia
g. Asiwe mbinafsi, kila wakati ajitolee kwa manufaa ya wengine kabla ya kufikiria atavyonufaika yeye.
h. Asitumie nafasi yake kwa faida yake, watu wenye nasaba naye au uswaiba
i. Awe msema kweli daima na fitina kwake mwiko
j. Awe ni mtu mwenye maarifa na ujuzi
k. Awe mwenye moyo wa kusamehe, asiwe mlipa kisasi
l. Asiwe na mabaya ya matumizi ya rasilimali zilizopo
m. Awe ni mtu jasiri katika kukabiliiana na changamoto za taasisi
n. Awe mbunifu, muwazi, mkweli na mwadilifu
o. Awe na uelewa kuhusu kanuni, sera, katiba, dire na dhima ya chama
p. Awe mpashanaji habari mzuri wa kutumia mikondo rasmi ya mawasiliano

q. Awe anajua kushughulikia mizozo, migongano na migogoro
r. Atambu kwamba binaadamu hutofautiana katika sifa na uwezo wa kufikiri, utashi,huluka, tabia na imani.
s. Asiwe na tama ya fedha
t. Awe na uwezo wa kuwaunganisha wanachama katika mambo yanayowahusu.

**MASHART YA UONGOZI:**

1. Awe na umri angalau miaka 18 na kuendelea
2. Asiwe mwajiliwa kwenye taasisi nyingine kwani atakosa muda wa kuwatumikia wanachama
3. Asiwe na kumbukumbu ya makosa ya jinai
4. Awe mtanzania kwa kuzaliwa
5. Awe amejiunga na chama angalau muda wa mwaka mmoja
6. Awe mwendesha pikipiki ya magurudumu mawili au matatu
7. Awe ameshakuwa kiongozi ngazi yoyote kuanzia kituo, kata na wilaya
8. Kiongozi ataruhusiwa kugombea nafasi yoyote ya uongozi kwa mihula miwili tu

**UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA WILAYA:**

6.1.3 Uchaguzi wa viongozi kwenye umoja

6.1.4 Mkutano mkuu wa uchaguzi

6.1.5 Mkutano mkuu wa uchaguzi utaitishwa baada ya miaka mitano (5) tarehe na mwezi wa uchaguzi vitapangwa na kamati kuu

6.1.6 Mkutano mkuu wa uchaguzi utaitishwa na katibu mkuu baada ya kushauriana na mwenyekiti wa chama

6.1.7 Mwenyekiti atafungua mkutano mkuu wa uchaguzi na kuwakaribisha wajumbe wa kamati ya uchaguzi wachukue nafasi yao.

**VIONGOZI WALIOKUWA MADARAKANI KUJIUZURU:**

6.1.8 Baada ya wajumbe wa kamati kujongea mbele, mwenyekiti wa umoja atatangaza kujiuzuri na hivyo kumaliza muda wa uongozi wake na vioongozi wengine waliokuwa chini yake

6.1.9 Viongozi ambao Kwa tangazo la mwenyekiti la kujiuzuri uongozi watakuwa ni:

- Mwenyekiti.
- Makamu mwenyekiti.
- Katibu.
- Naibu katibu.
- Mhasibu/au mweka hazina.
- Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu.
- Naibu msimamizi wa nidhamu.

6.1.10 viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi ngazi husika wataondoka meza kuu na kamati ya uchaguzi watachukua nafasi ili kusimamia uchaguzi.

6.1.11 Mchakato wa kuwapata viongozi utaanza baada ya mhula wa kwanza wa viongozi walioko madarakani kumalizika

6.1.12 Mchakato wa uchaguzi wa kuwapata viongozi ngazi ya wilaya utaanzia kwenye kata kwa kutangaziwa na kamati ya uchaguzi kuchukua fomu mwezi mmoja kabla ya uchaguzi huo.

6.1.13 Viongozi wa kata watawatangazia wanachama wao kuchukua fomu toka kwa voingozi hao

6.1.14 Viongozi wa kata wataitisha mkutano mkuu wa kata kwa ajili ya kufanya mchakato wa kupata majina sita (6) ya wagombea ngazi ya wilaya.

6.1.15 Baada ya mchakato huo wa mchujo majina hayo yaliyopitishwa, viongozi wa kata watayawasilisha kwenye kamati ya uchaguzi ngazi ya wilaya wiki moja kabla ya uchaguzi

6.1.16 Katika kupendekeza majina kata haita:

a) Haitapendekeza mwanachama ambaye hajamaliza mwaka mmoja tangu ajiunge na umoja
b) Haitapendekeza mwanachama ambaye ametumikia vipindi viwili katika nafasi hiyo hiyo
c) Haitapendekeza mwanachama aliyefukuzwa uongozi au aliyeshinikizwa kujiuzuru kwa makosa aliyoyatenda akiwa kiongozi
d) Haitapendekeza mwanachama ambaye hajui kusoma na kuandika
e) Haitapendekeza mwanachama ambaye hafanyi kazi nje ya wilaya ya Arusha
f) Haitapendekeza mwanachama ambaye siyo mwanachama hai

6.1.17 Makatibu wa kata watakabidhi majina ya wagombea kwa katibu mkuu Wilaya yaliyopendekezwa

**KATIBU MKUU KUKABIDHI MAJINA YA WAGOMBEA KWA KAMATI YA UCHAGUZI:**

6.1.18 Baada ya katibu mkuu kupokea majina ya wagombea waliopendekezwa na kata kugombea uongozi ndani ya siku zisizozidi saba (7) katibu mkuu atawajibika:

a) Kutengeneza orodha ya wagombea kwa utaratibu unaofaa
b) Kutuma kwenye kata majina ya wagombea wote waliopendekezwa
c) Kuandika barua ya kuwasilisha (covering leter) majina ya wagombea kwa mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi na
d) Kuwasilisha kuwasilisha majina kwa mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi

6.1.19 Mapema iwezekanavyo na kabla ya kamati ya uchaguzi kufanya kikao cha kujadili na kupitisha wagombea kwa kila nafasi:

6.1.20 Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atahifadhi mahala pa usalama majina ya wagombea kama alivyoyapokea toka kwa katibu mkuu mpaka:

a) Atakapokubaliana na kushauriana na katibu wa kamati ya uchaguzi kuitisha kikao cha cha uteuzi wa mwisho wa wagombea.

b) Kikao cha kamati ya uchaguzi cha uteuzi wa wagombea kitakaa ndani ya siku saba (7) kabla ya siku ya uchaguzi na kuchuja majina ya wagombea
c) Akidi ya kikao itakuwa ni 50%
d) Ili kuzuia kampeni, majina ya wagombea waliopitishwa kwa kila nafasi na wale walioachwa yatabaki siri ya kamati ya uchaguzi mpaka mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atakapofungua bahasha na kusoma majina ya wagombea waliopitishwa

**KUTEUA WAGOMBEA WA UONGOZI:**

6.1.21 Kutoka kwenye majina yaliyopitishwa katika mkutano mkuu wa kata, kamati ya uchaguzi itapitisha majina ya wagombea majina matano (5) kwa kila nafasi ya:

- Mwenyekiti.
- Makamu mwenyekiti.
- Katibu.
- Naibu katibu.
- Mhasibu/au mweka hazina.
- Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu.
- Naibu msimamizi wa nidhamu.

6.1.22 Katika kuchambua, kujadili na kupitisha majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wajumbe wa kamati wanawajibika:

a) Kuzingatia maslahi mapata ya chama
b) Kuzingatia uwezo wa kila mgombea katika kutumikia kila nafasi aliyoomba na si
c) Kutunza siri za majadiriano na uamuzi ili kuzuia uwezekano wa kampeni

6.1.23 Kamati ya uchaguzi katika kujadili na kuteua wagombea wa uongozi wa chama inakatazwa kujihusisha na:

a) Ushabiki, ubaguzi wa jinsia au ubaguzi mwingine wa moja kwa moja au usiokuwa wa moja kwa moja
b) Ushawishi wa viongozi au mtu yeyote ambaye siye mjumba wa kamati
c) Maslahi binafsi, undugu, ukabila au nasaba
d) Mitazamo ya kisiasa, mwegemeo wa imani za kidini na hali ya mtu kijamii
e) Ubaguzi kwa misingi ya eneo analotoka mgombea

6.1.24 Majina ya wagombea yaliyopitishwa kwa kila nafasi yatawekwa kwenye bahasha ambayo:

a. Itafungwa ipasavyo
b. Juu yake itaandikwa nafasi ambayo wagombea wamepitishwa kugombea
c. Itakabidhiwa kwa mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi baada ya kugawa karatasi za kura kabla ya kupiga kura kwa nafasi husika

6.1.25 Kamati ya uchaguzi haitagawa karatasi za kupiga kura mpaka:

a. Wageni na wanachama wasiokuwa hai wametengewa nafasi maalumu ili wasipige kura
b. Wanachama ambao hawajatimiza mwaka mmoja tangu wajiunge wametambuliwa na wametambulishwa kwa wapiga kura ili wasichaguliwe
c. Wanachama wenye sifa za kupiga kura wamehesabiwa ipasavyo na

d. Wapigakura waliohudhuria siyo chini ya asilimia 60% ya wanachama wote kwa mujibu wa utaratibu wa upigaji kura

6.1.26 Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi hatafungua bahasha yenye majina ya wagombea wa nafasii husika mpaka:

a. Ajiridhishe kwamba bahasha inayofunguliwa imeandikwa juu yake nafasi yake inayogombewa
b. Karatasi za wapiga kura zimegawiwa ipasavyo kwa idadi ya wapiga kura
c. Amejiridhisha kwamba hakuna mazingira ya kupiga kampeni kabla na baada ya kutangaza wagombea
d. Amejiridhisha kwamba wapiga kura wako tayari kupiga kura
e. Baada ya kujiridhisha mwenyekiti wa uchaguzi atafungua bahasha kuwasoma majina na kuwatangaza wagombea wa nafasi ambayo wapigakura wametayarishwa kuchagua

6.1.27 Viongozi watachaguliwa kwa mtiririko ufuatao:

- Mwenyekiti
- Makamu mwenyekiti
- Katibu
- Naibu katibu
- Mhasibu/au mweka hazina
- Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
- Naibu msimamizi wa nidhamu

**UTARATIBU WA UPATIKANAJI WA KAMATI MBALIMBALI:**

6.1.28 Kamati mbalimbali zitapatikana kwa kupendekezwa na kamati kuu na kupitishwa na Halmashauri kuu.

6.1.29 Halmashauri itapitisha:

a. Wajumbe watano (5) wa kamati ya nidhamu na maadili
b. Wajumbe watano (5) wa kamati ya uchumi na fedha
c. Wajumbe wa kamati ya uchaguzi watakuwa ni watu 6
d. Wajumbe wa kamati maalum watakuwa ni watano (5)

6.1.30 Kingozi yeyote wa chama hatakiwi kuwa na nafasi mbili za uongozi

6.1.31 Kamati mbalimbali zitapatikana baada ya uchaguzi mkuu ndani ya miezi mitatu (3)

6.1.32 Baada ya kukubaliana na kushauriana na mwenyekiti, lakini kabla ya uchaguzi wa viongizi wa kamati mbalimbali katibu mkuu atawateua makatibu wa kamati mbalimbali toka miongoni mwa wajumbe wa kamati waliopendekezwa na halimashauri.

**Wasimamizi wa uchaguzi kwenye kata na kamati za kikatiba:**

6.1.33 Viongozi wa kamati kuu au viongozi wengine watakao teuliwa na kamati kuu watasimamia uchaguzi wa viongozi wa kamati za kikatiba na viongozi wa kata

**Utaratibu wa uchaguzi wa viongozi wa kata.**

6.1.34 Uchaguzi wa kata utafuata utaratibu ufuatao:

a. Akidi ya mkutano wa uchaguzi wa kata itakuwa ni wajumbe wasiopungua asilimia 75% ya wapiga kura wote kwenye kata
b. Kila mwanachama wa kata ana haki ya kugombea nafasi ya uongozi kwenye kata husika
c. Wajumbe wa mkutano wa uchaguzi wa kata watapiga kura za siri
d. Kura za papo kwa papo zitapigwa, na atakayepata kura nyingi lakini zisiwe chini ya asilimia 50% ya kura zilizopigwa ndiye atakayekuwa amechaguliwa
e. Wapiga kura kwenye kata watachagua:
    - ✓ Mwenyekiti
    - ✓ Makamu mwenyekiti
    - ✓ Katibu
    - ✓ Naibu katibu
    - ✓ Mhasibu/au mweka hazina
    - ✓ Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
    - ✓ Naibu msimamizi wa nidhamu

F viongozi wa kata wataanza kutekeleza majukumu ya uongozi mara tu baada ya kusimikwa rasmi

**KUWASIMIKA VIONGOZI**

**6.1.35** Kusimika viongozi:

a. Mshindi wa nafasi ya uongozi atatangazwa kabla ya kuchagua nafasi ya kiongozi anayefuata
b. Uchaguzi ukisha kamilika, mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atawaalika viongozi wateule kujongea mbele
c. Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atawaalika mkutano mkuu wa uchaguzi kushangilia viongozi wateule
d. Kushangilia viongozi ni kuashilia kwamba viongozi wateule sasa wamesimikwa rasmi
e. Mkutano Mkuu Utaratibu uliotajwa kwenye kifungu A utatumika kuwasimika viongozi kwenye kata, vituo, kamati za kikatiba

**UTARATIBU WA UCHAGUZI KWENYE KITUO.**

Uchaguzi wa kituo utafuata utaratibu ufuatao:

f. Akidi ya mkutano wa uchaguzi wa kituo itakuwa ni wajumbe wasiopungua asilimia 75% ya wapiga kura wote kwenye kituo
g. Kila mwanachama wa kituo ana haki ya kugombea nafasi yeyote ya uongozi kwenye kituo husika
h. Wajumbe wa mkutano wa uchaguzi wa kituo watapiga kura za siri
i. Kura za papo kwa papo zitapigwa, na atakayepata kura nyingi lakini zisiwe chini ya asilimia 50% ya kura zilizopigwa ndiye atakayekuwa amechaguliwa
j. Wapiga kura kwenye kituo watachagua:
    - ✓ Mwenyekiti
    - ✓ Makamu mwenyekiti
    - ✓ Katibu
    - ✓ Naibu katibu
    - ✓ Mhasibu/au mweka hazina

- ✓ Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
- ✓ Naibu msimamizi wa nidhamu

F viongozi wa kituo wataanza kutekeleza majukumu ya uongozi mara tu baada ya kusimikwa rasmi

**ADHABU MBALIMBALI ZA WANACHAMA KWENYE CHAMA**:

Kutakuwa na adhabu mbalimbali kwenye chama kuanzia ngazi zifuatazo;

(a) Ngazi ya wilaya.
(b) Ngazi ya kata.
(c) Ngazi ya kituo.

**ADHABU NGAZI YA WILAYA:**

Mwanachama anaweza kuadhibiwa ngazi ya wilaya endapo ataonekana ametenda yafuatayo;

(a) Amedharau Uongozi wa wilaya au maelekezo yoyote yaliyotolewa Kwa mujibu wa katiba.
(b) Ni marufuku mwanachama au kiongozi yeyote kwenye umoja kuwa na hali ya Ubaguzi kama vile; ukabila, udini, siasa n.k.
(c) Atatoa lugha ya matusi, kupigana akiwa kwenye eneo lake la kazi lkn pia na kwa wateja wake.
(d) Ni marufuku kwa mwanachama yoyote kupaki kwenye kituo ambacho si ofisi yake ya kufanyia kazi yaani (Mvamizi)
(e) Halipi ada au michango mbalimbali ndani chama.
(f) Ni marufuku kwa mwanachama yoyote wa umoja aliye na kituo au asiye na kituo kupaki kwenye eneo lolote ambalo halina kituo ndani ya wilaya.
(g) Ni marufuku kutumia vitu vifuatavyo unapokuwa kwenye eneo la kazi kama vile: Bangi, Pombe, Mirungi, Unga, Sigara n.k.
(h) Ni marufuku wanachama kushawishi maandamano au mgomo na wanachama wenzake pindi akiwa kwenye eneo lake la kazi bila ruhusa ya viongozi wake.
(i) Kutoudhuria vikao ngazi ya wilaya.

(a) Ni marufuku mwanachama kufanya mambo yafuatayo ndani ya wilaya:
(a) Kunyanyua tairi ya mbele ya pikipiki juu.
(b) Kupiga norinda
(c) Kupiga resi.

(j) Ni marufuku mwanachama yoyote kujihusisha na mambo yafuatayo Kama vile: wizi wa kutumia pikipiki, uporaji (Tatu mzuka) ndani ya wilaya.
(k) Ni marufuku mwanachama yoyote kumtania mwanachama mwenzake kwa maneno ya kashfa na kejeli.
(l) Ni marufuku mwanachama yoyote kumtolea abiria maneno ya kashfa na kejeli.
(m) Ni marufuku kwa mwanachama yoyote kutofuata utaratibu wa ubebaji abiria.
(n) Ni marufuku mwanachama kufanya mambo yafuatayo kwenye kituo:
(o) Ni marufuku mwanachama kubeba abria zaidi ya mmoja yaani (Mshikaki).

(p) Ni marufuku mwanachama yoyote kuhamasisha mgomo au maandamano Kwa wanachama wenzake akiwa kwenye eneo lake la kazi bila ruhusa ya viongozi.

**ADHABU NGAZI YA KATA:**

Mwanachama anaweza kuadhibiwa ngazi ya Kata endapo ataonekana ametenda yafuatayo;

(b) Amedharau uongozi wa Kata au maelekezo yoyote yaliyotolewa kwa mujibu wa katiba
(c) Atatoa lugha ya matusi, kupigana akiwa kwenye eneo lake la kazi lkn pia na kwa wateja wake.
(d) Ni marufuku mwanachama au kiongozi yeyote wa umoja kwenye kata kuwa na hali ya Ubaguzi kama vile; ukabila, udini, siasa n.k.
(e) Ni marufuku mwanachama yoyote kutolipa ada au michango mbalimbali ndani ya kata husika.
(f) Ni marufuku kwa mwanachama yoyote wa umoja aliye na kituo au asiye na kituo kupaki kwenye eneo ambalo halina kituo ndani ya kata husika.
(g) Ni marufuku kwa mwanachama yoyote kupaki kwenye kituo ambacho si ofisi yake ya kufanyia kazi yaani (Mvamizi).

(h) Ni marufuku kutumia vitu vifuatavyo unapokuwa kwenye eneo la kazi kama vile; Bangi, Pombe, Mirungi, Unga, Sigara n.k.
(i) Ni marufuku Kwa mwanachama yoyote kutofuata utaratibu wa ubebaji abiria ndani kata husika.
(j) Ni marufuku mwanachama kufanya mambo yafuatayo ndani ya kata husika:
  (d) Kunyanyua tairi ya mbele ya pikipiki juu.
  (e) Kupiga norinda
  (f) Kupiga resi.
(k) Ni marufuku mwanachama yoyote kuhamasisha mgomo Kwa wanachama wenzake akiwa kwenye eneo lake la kazi bila ruhusa ya viongozi
(l) Kutoudhuria vikao ngazi ya kata.
(m) Ni marufuku mwanachama yoyote kujihusisha na mambo yafuatayo Kama vile: wizi wa kutumia pikipiki, uporaji (Tatu mzuka) ndani ya kata husika.
(n) Ni marufuku mwanachama yoyote ndani ya kituo kumtania mwanachama mwenzake kwa maneno ya kashfa na kejeli.
(o) Ni marufuku mwanachama yoyote kumtolea abiria maneno ya kashfa na kejeli.
(p) Ni marufuku mwanachama kubeba abiria zaidi ya mmoja yaani (Mshikaki).

**ADHABU NGAZI YA KITUO:**

Mwanachama anaweza kuadhibiwa ngazi ya kituo endapo ataonekana ametenda yafuatayo;

(a) Amedharau uongozi au maelekezo yaliyopo kwa mujibu wa katiba ngazi ya kituo.
(b) Atatoa lugha ya matusi, kupigana akiwa kwenye eneo lake la kazi lkn pia na kwa wateja wake.
(c) Ni marufuku mwanachama au kiongozi yeyote kwenye umoja kuwa na hali ya Ubaguzi kama vile; ukabila, udini, siasa n.k.
(d) Halipi ada au michango mbalimbali akiwa ni mwanachama kwenye kituo chake.
(e) Kupaki kwenye eneo ambalo halina kituo.
(f) Kupaki kwenye kituo ambacho si ofisi yake ya kufanyia kazi yaani (Mvamizi).

(g) Ni marufuku kutumia vitu vifuatavyo unapokuwa kwenye eneo la kazi kama vile; Bangi, Pombe,Mirungi, Unga , Sigara n.k.
(h) Kutofuata utaratibu wa kituo husika katika ubebaji abiria.
(i) Ni marufuku mwanachama kufanya mambo yafuatayo kwenye kituo:
 (g) Kunyanyua tairi ya mbele ya pikipiki juu.
 (h) Kupiga norinda
 (i) Kupiga resi.
(j) Mwanachama kuhamasisha mgomo na wenzake pindi akiwa kwenye eneo lake la kazi.
(k) Kutoudhuria vikao ngazi ya kituo, kata, wilaya.
(l) Ni marufuku mwanachama yoyote kujihusisha na mambo yafuatayo Kama vile: wizi wa kutumia pikipiki, uporaji (Tatu mzuka) ndani ya kata husika.
(m) Ni marufuku mwanachama yoyote ndani ya kituo kumtania mwanachama mwenzake kwa maneno ya kashfa na kejeli.
(n) Ni marufuku mwanachama yoyote ndani ya kituo kumtolea abria maneno ya kashfa na kejeli.
(o) Ni marufuku mwanachama kubeba abria zaidi ya mmoja yaani (Mshikaki).

**SURA YA SABA:**

**3.1.1 MFUKO WA UMOJA.**

7.1.1 Mfuko wa Umoja utakuwa na maana ya Mfuko Mkuu wa Umoja

A. **Mfuko wa Wilaya**
B. **Mfuko wa Kata**
C. **Mfuko wa Kituo**

**Mfuko wa Wilaya:**

7.1.2 Mfuko wa Wilaya utaundwa na Kata zote ishirini na tano (25) za Wilaya ya Arusha Mjini

- **Mfuko huu wa Wilaya utakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo:**

1. Ada za wanachama za kila mwezi itakuwa ni kiasi kiilichoainishwa kwenye kanuni
2. Viingilio vya wanachama wapya watakaojiunga na Umoja;
3. Adhabu za papo kwa papo;
4. Adhabu zinazotokana na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili
5. Kutunisha mfuko kwa njia ya;
6. Harambee;
7. Mnada;
8. Faida itokanayo na mikopo;

9. Faida itokanayo na uwekezaji; (miradi)
10. Misaada kutoka kwa watu binafsi au taasisi; na
11. Mauzo ya Katiba ya chama
12. Mauzo ya form za fursa mbalimbali
13. Vyanzo vingine vya mapato,

7.1.3 **Mfuko wa Kata**

- **Mfuko wa Kata utaundwa na vituo vyote ndani ya Kata husika**
  Mfuko huu wa kata utakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo:

1. Viingilio vya wanachama wapya watakaojiunga na Umoja ngazi ya Kata
2. Adhabu za papo kwa papo
3. Adhabu zinazotokana na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili
4. Kutunisha mfuko kwa njia ya
5. Harambee
6. Mnada
7. Faida itokanayo na mikopo;
8. Faida itokanayo na uwekezaji; (miradi)
9. Misaada kutoka kwa watu binafsi au taasisi; na
10. Vyanzo vingine vya mapato

7.1.3 **Mfuko wa Kituo,**

- Mfuko huu wa kituo utakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo:

1. Viingilio vya wanachama wapya watakaojiunga na Umoja ngazi ya Kituo
2. Adhabu za papo kwa papo
3. Adhabu zinazotokana na uamuzi wa kituo
4. Faida itokanayo na mikopo;
5. Vyanzo vingine vya mapato

7.1.4 **Masharti yafuatayo yatatawala uwekaji fedha kwenye mfuko mkuu wa Umoja:**

A. Uongozi wa kituo utakusanya ada kutoka Kwa wanachama wao kulingana na idadi ya wanachama wao kwenye kituo.
B. Baada ya makusanyo hayo, mweka hazina wa kituo ataweka fedha hizo kwenye akaunti ya chama ngazi ya wilaya, kisha baada ya kuweka fedha hizo atalazimika kuwasilisha risiti hiyo Kwa mweka hazina wa kata husika.
C. Fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya mfuko mkuu zitawekwa kwenye akaunti za umoja;
D. Malipo yote yaliyofanyika ngazi ya kituo, na kata yatakatiwa stakabadhi na mweka hazina wa wilaya ambayo pekee ndiyo uthibitisho wa malipo hayo;
E. Malipo ya tahesabika kuwa yamefanyika baada ya kupokea stakabadhi ya Umoja ngazi ya wilaya;
F. Hela itatolewa kwenye akaunti pamoja na hundi kwa watia saini wawili kati ya watatu
G. Watia saini kwenye akaunti pamoja na hundi watachaguliwa na Halmashauri ya Umoja;
H. Watia saini kwenye akaunti ya umoja wawe wanaweza kupatikana Kwa urahisi.
I. Mifuko yote ya umoja kuanzia kituo na kata, itakuwa chini ya usimamizi wa Umoja Mkuu

7.1.5 Mazingira **yanayoruhusiwa kupokea Fedha Taslim;**

Viongozi wanaruhusiwa kupokea fedha taslimu inayotokana na:
(a) Mnada na ambayo imelipwa wakati mnada unaendelea au mara tu
Baada ya kumalizika;
(b) Harambee wakati inaendelea au mara tu baada ya kumalizika;
(c) Malipo yoyote yaliyofanywa na mtu ambaye siyo mwanaumoja;
(d) Zawadi iliyotolewa papo hapo; na
(e) Fedha nyingine ambayo itapokelewa Kwa mazingira yaliyoruhusiwa na
Halmashauri.
Bila kuathiri vifungu vingine vya katiba, itakuwa kinyume cha masharti ya Katiba
Hii Kwa:
(a) Mwanaumoja yeyote kulipa fedha taslim Kwa kiongozi; na
(b) Kiongozi yeyote kupokea fedha taslim kutoka Kwa mwanaumoja
Yeyote.
Kiongozi atakayekiuka katazo la kupokea fedha taslim:
(a) Atakuwa ametenda kosa;
(b) Atafikishwa mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
(c) Atawajibika kutekeleza uamuzi wa Kamati ya Nidhamu.

**MATUMIZI YA MFUKO WA UMOJA MKUU:**
Matumizi ngazi ya wilaya yatakuwa Kama ifuatavyo:

a. Kulipa kodi ya pango ya kila mwezi ya ofisi
b. Uendeshaji wa gharama za ofisi
c. Gharama za maandalizi ya mikutano.
d. Posho za vikao
e. Posho za utatuzi wa migogoro ya wanachama
f. Gharama za Safari za viongozi
g. Kuhudumia wanachama katika ajali na vifo vinavyotambulika kikatiba
h. Malipo ya mishahara kwa waajiriwa na chama
i. Malipo ya kuendeshea kesi katika kulinda haki za Chama na mwanachama
j. Malipo ya adhabu yoyote iliyotoiewa dhidi ya Chama
k. Uwekezaji Kama itakavyoamuliwa na chama.
l. Malipo ya ushirikishwaji wa Chama.
m. Malipo mengine halali kwa manufaa ya chama
n. Malipo ya mafunzo na semina kwa viongozi na wanachama wenyewe

**Matumizi ya mfuko ngazi ya kata yatakuwa Kama ifuatavyo:**

a. Kulipa kodi ya pango ya kila mwezi ya ofisi
b. Uendeshaji wa gharama za ofisi
c. Gharama za maandalizi ya mikutano
d. Posho za vikao
e. Posho za utatuzi wa migogoro ya wanachama
f. Gharama za Safari za viongozi
g. Kuhudumia wanachama katika ajali na vifo vinavyotambulika kikatiba
h. Uwekezaji Kama itakavyoamuliwa na chama.
i. Malipo mengine halali kwa manufaa ya chama

**Matumizi ya mfuko ngazi ya Kituo yatakuwa Kama ifuatavyo:**

a. Gharama za maandalizi mkutano wa kituo
b. Posho za viongozi wa kituo wanapoitwa kwenye vikao vya chama
c. Posho za viongozi wa kituo wakati wa utatuzi wa migogoro ya wanachama wao
d. Kuhudumia wanachama katika ajali na vifo vinavyotambulika kikatiba
e. Malipo mengine halali kwa manufaa ya chama

- 7.1.6 **Taarifa ya Mapato Na Matumizi;**

Mweka Hazina ataandaa taarifa ya mapato ikihusisha fedha yote iliyopatikana
Kutokanana:
(a) Ada ya Umoja ya kila mwezi;
(b) Kila adhabu;
(c) Harambee;
(d) Kutunisha mfuko;
(e) Viingilio;
(f) Faida inayotokana na kuweka fedha benki;
(g) Faida inayotokana na kuwekeza kwenye SACCOS; na
(h) Vyanzo vingine.
Mweka Hazina ataandaa taarifa yamatumizi ikihusisha:
(a) Matumizi ya vikao na mikutano ya Umoja;
(b) Matumizi Kwa kila huduma;
(c) Gharama za benki;
(d) Gharama za ukaguzi wa hesabu; na
(e) Matumizi mengine.

7.1.7 **Ukaguzi wa Mapato na Matumizi ya Mfuko Mkuu**

Mwaka wa fedha wa Umoja unaanza tarehe 1 Julai na kuisha tarehe 30 Juni kila
mwaka.
Hesabu za Umoja zitakaguliwa na taarifa kutolewa na wakaguzi wenye taaluma
Ya ukaguzi kutoka aidha miongoni mwawanaumoja au njeya Umoja:
(a) Ndani ya miezi mitatu tangu kufunga mwaka wafedha;
(b) Wakaguzi watakabidhi taarifa kwa Kamati Kuu mara tu baada ya
Kumaliza kukagua;
(c) Kamati Kuu itawasilisha taarifa ya ukaguzi kwenye kikao cha kawaida
cha Halmashauri au cha dharura ili wakaguzi wawasilishe taarifa ya
ukaguzi na kiufafanua;
(d) Halmashauri itaijadili kwa kina kabla ya kuwasilishwa kwenye Mkutano
Mkuu

- **Kima cha Chini cha Mfuko Mkuu na Matumizi yake;**

Muda wowote ule mfuko wa Umoja utakuwa na kiasi cha fedha
Kilichoidhinishwa na Mkutano Mkuu kuwa kima cha chini. Fedha itahesabika
Kuwa ni sehemu ya fedha iliyopo kwenye mfuko wa Umoja iwapo:
(a) Ipo kwenye akaunti za Umoja;
(b) Ipo kwenye mikopo ya muda mfupi; na
(c) Imewekezwa kwenye SACCOS kama Amana.
Mfuko mkuu wa Umoja utatumika kwa mambo yafuatayo:
(a) Kutoa huduma zilizoainishwa na katiba hii na viwango vyake kutajwa
Kwenye kanuni;
(b) Kugharamia vikao vya Umoja na uendeshaji wa Umoja;
(c) Uwekezaji kwenye SACCOS; na
(d) Uwekezaji kwenye miradi.
7.1.8 **MAFUKO WA BODABODA KATA:**

(a) Ada ya kituo ya kila mwezi ambayo imeidhinishwa na Kamati Kuu kwa maandishi; na
(b) Mchango mwingine ambao kituo itaomba kwa maandishi na Kamati Kuu Kuuidhinisha kwa maandishi.
(a) Haitawekwa kwenye akaunti ya mfuko mkuu wa Umoja; na
(b) Itatumika kwaajili ya matumizi madogomadogo ya Kata kadiri Yatakavyo ainishwa na kanuni.
Mikopo kwenye Umoja
Umoja utatoa mikopo midogomidogo kwa wanaumoja kwa mashartiya fuatayo:
(a) Muda wa kulipa mkopo na riba yake ni miezi minne;
(b) Mkopo utarejeshwa katika marejesho manne kwa utaratibu wa kurejesha Kila mwezi 25% au zaidi ya mkopo wote pamoja na riba; na
(c) Mkopo utatozwa riba yaasilimia 10 kwa kipindi chote cha miezi minne.
Mkopo hautatolewa mpaka:
(a) Mwanaumoja awe ametimiza mwaka mmoja tangu kujiunga na Umoja;
(b) Mkopaji awe amejaza fomu ya maombi ya mkopo na kudhaminiwa na Wadhamini wasiopungua wawili;
(c) Kamati Kuu iwe imejiridhisha kwamba mkopaji hajawahi kushindwa kulipa mkopo;
(d) Kama aliwahikushindwa kulipa mkopo ithibitike kwamba alishalipa hela ya Wadhamini ambayo walimlipia kwa mkopo alioshindwa kurejesha;
(e) Mkopaji na wadhamini wake wawe wanaumoja hai; na
(f) Awe nauwezo wa kurejesha.
Kuchelewesha Mkopo
Atakayecheleweshа mkopo:
(a) atatozwa adhabu ya asilimi 10 ya mkopo wote pamoja na riba yake iwapo Atalipa ndani ya siku thelathini tangu muda wakawaida wakulipa mkopo kuisha;
(b) mweka-Hazina atawajulisha wadhamini wa mkopaji baada ya mkopo kucheleweshwa siku 10;
(c) mkopaji na wadhamini watawajibika kulipa mkopo, riba na adhabu ndani ya siku 30 tangu muda wakawaida wa kulipa kuisha;
(d) siku 30 zikiisha bila kulipa mkopo mkopaji na wadhamini watafungiwa Huduma kwa kushindwa kulipa Mkopo
Iwapowadhamini watalipa mkopo kabla au baada ya kufungiwa huduma:
(a) kwa maombi ya wadhamini mkopaji ataendelea kufungiwa huduma;
(b) kwa maombi ya wadhamini atafikishwa Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
(c) kama mkopaji ni kiongozi atapoteza nafasi yake ya uongozi

**MAREKEBISHO YA KATIBA**

**Katiba hii na vipengele vyake vinaweza kurekebishwa na mkutano mkuu iwapo theluthi mbili 2/3 ya wanachama waliohudhuria watapapiga kura ya kuunga mkono wa urekebishwaji huo.**

Mabadiliko ya Katiba yatafanyika kila baada ya miaka mitano.

Kamati Kuu itaunda Kamati ya Katiba na kuwasilisha majina ya

Wajumbe kwenye Halmashauri ya Umoja ambayo:

(a) Inaweza kubadilisha muundo, idadi na aina ya wajumbe wa Kamati ya katiba iwapo

Kuna sababu za msingi; na

(b) Itaridhia iwapo hakuna sababu za msingi za kufanya mabadiliko.

Kamati ya Katiba itaanza kazi rasmi mara baada ya kuridhiwa na Halmashauri;

Kamati ya Katiba itakamilisha kazi ya kuandika rasimu ya katiba na katiba

Itapitishwa na Mkutano Mkuu.

Maoni ya marekebisho ya Katiba yatakusanywa kwa utaratibu ufuatao-

(a) Mwanaumoja atawasilisha kwa katibu wa Kata yake maoni ya marekebisho ya katiba

Kwa maandishi muda wowote anapogundua mapungufu kwenye katiba inayotumika;

(b) Katibu wa kata ataweka maoni ya mwanaumoja mahala pa usalama;

(c) Katibu wa Kata atawasilisha maoni hayo kwa Kamati ya Marekebisho ya Katiba muda wa kurekebisha Katiba utakapowadia; na

(d) Mwanaumoja atafuatilia kuhakikisha kwamba Kamati ya Kurekebisha Katiba

Imepokea maoni yake; na

(e) Kamati ya Katiba itaweka utaratibu muafaka kwaajili ya kupata maoni kutoka kwa wanaumoja wengi kadri iwezekanavyo.

Iwapo kwa sababu zozote zile idadi ya wajumbe wa Kamati ya Katiba itapungua-

(a) Kamati Kuu itaongeza wajumbe kulingana na idadi ya wajumbe waliopungua;

(b) Kama hakuna kikao cha Kamati Kuu kinachotarajia kuitishwa ndaniya siku 15 tangu

idadiya wajumbe kupungua, Katibu Mkuu baada ya kushauriana na Mwenyekiti

atateua wajumbe kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Katika marekebisho ya katiba Kamati inashauriwa kuwa na mashauriano ya takayosaidia Kufikia makubaliano kwa muafaka na maelewano. Iwapo hili halitawezekana:

(a) Makubaliano yatafikiwa kwa njia ya kupiga kura; na

(b) Iwapo kura zitagawanyika nusu kwa nusu mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Katika kupitisha vifungu vya katiba na hatimaye katiba nzima, vifungu ambavyo vitazua

Mabishano-

(a) Wanaumoja watazingatia maelezo ya wajumbe wa Katiba;

(b) Iwapo kuna haja Kura zitapigwa na kifungu kitapitishwa kwa kura za wanaumoja

Wengi; na

(a) Kamati ya marekebisho ya katiba itaingiza nyongeza ya vifungu vilivyoamuliwa na Mkutano Mkuu;

(b) Isipokuwa makosa yakiuchapishaji tu, kamati ya katiba haitafanya marekebisho

Yoyote kwenye katiba iliyopitishwa na MkutanoMkuu.

Baada ya Kamati ya Katiba kumaliza kuandaa katiba iliyopitishwa:

(a) Mwenyekiti na Katibu Mkuu watatia saini zao kwenye Katiba kuthibitisha kupitishwa Kwake kwenye Mkutano Mkuu; na

(b) Katiba iliyosainiwa kwenye nakala za kutosha itawasilishwa kwa mamlaka zinazohusika Ili isajiliwe.

Kuanza kutumika Kwa Katiba hii

Katiba hii imepitishwa na wanaumoja kwenye Mkutano Mkuu na kuanza kutumika leo

siku ya......................mwezi wa.......................................

................................................................................ ......

**MWENYEKITI (W) …………………………………………………..**

**KATIBU MKUU(W)…………………………………………………**

**MWEKAHAZINA(W)………………………………………………**